# *Mume Mpya, Mke Mpya,*

# *Maisha Mapya*

---

Mafundisho ya Biblia, Kuhusu Ndoa, Familia na Jinsia

Swahili (Kenyan) Edition

---

Na Carrie A. Miles, Ph.D.
Pamoja na Laurence R. Iannaccone, PhD.
Kimetafsiriwa na Apostle David Barasa Wanyonyi

Tafsiri ya Kiswahili
Kimeandikwa na Carrie A.Miles 2012. Haki zote zimehifadhiwa.
Kimechapiswa na Empower International Ministries.
www.EmpowerInternational.org

# Mume Mpya, Mke Mpya, Maisha Mapya

Biblia inatoa sehemu tatu za hadithi ya uhusiano wa mwanadamu na Mungu pamoja na wenzake. “Hapo zamani za kale” Hadithi hii inatufunulia Kwamba, wanadamu waliumbwa mume na mke kwa sura ya Mungu, kutimiza wazo kwamba-mwili mmoja, uchi na ndoa isiyo na aibu ambayo ni kilele cha kitendo cha uumbaji. Sehemu ya pili ya hadithi inatuonyesha kukataa kwetu maisha ya imani na kupoteza kipaji cha milele cha Mungu kwa ajili yetu. Anguko hili kutoka kwa neema lilileta utengano kati ya viumbe vya Mungu, kung’ang’ania mamlaka juu ya wenzake na kupoteza upendo usio na aibu ambao Mungu alituumbia .Sehemu ya mwisho ya hadithi hii tunapata kukombolewa, tumerejeshwa na Kristo kutoka kwa utumwa wa ulimwengu ulioanguka ambamo tulijiuza sisi wenyewe.

Kitabu hiki cha mwelekeo huchambua hadithi hii kikionyesha jinsi ukombozi sio tu kuturejesha kila mmoja wetu kwa umoja na Mungu, bali huturejesha kwa wazo la kuumbwa la umoja na kulingana na mmoja.Kupitia kwalo tunafanyika mume mpya, mke k waliorejeshwa kwa maisha mapya katika Kristo.

## Meza ya Yaliomo


Mume Mpya, Mke Mpya, Maisha Mapya ..... 2

SOMO LA 1 MUME NA MKE HAPO MWANZO ..... 3

SOMO LA 2 UHUSIANO WENYEWE ..... 5

SOMO LA 3 NAFASI YA MUME NA MKE KWA MUNGU ..... 8

SOMO LA 4 MWISHO WA UMOJA ..... 11

SOMO LA 5 UKOMBOZI KUTOKA KWA LAANA ..... 15

SOMO LA 6 HESHIMA UTAWALA NA KUTIISHA ..... 18

SOMO LA 7 INAMAANISHA NINI KUWA BWANA? ..... 23

SOMO LA 8 UHURU AMBAO KRISTO ANAWAPA WANAWAKE ..... 26

SOMO LA 9 WANAWAKE WACHAFU ..... 28

SOMO LA 10 PAULO NA MAMLAKA NYUMBANI ..... 32

SOMO LA 11 MTUME PAULO NA “UBWANA ” ..... 37

SOMO LA 12 UNYENYEKEVU ..... 42

SOMO LA 13 SIRI YA NDOA ..... 45

WALIOCHANGIA ..... 48




© Carrie A. Miles, 2012

# SOMO LA 1 MUME NA MKE HAPO MWANZO

## MATHAYO MTAKATIFU 19:3-8.

> Basi Mafarisayo wakamwendea [Yesu]! Ni halali mtu kumwacha mkewe kwa kila sababu? Akajibu, akawambia, hamkusoma ya kwamba yeye aliyewaumba mwanzo, aliwaumba mtu mume na mtu mke, akasema, kwa sababu hiyo, mtu Atamwacha babaye na mamaye, ataambatana na mkewe, na hao wiwili watakuwa mwili mmoja? Hata wamekuwa si wawili tena, bali mwili mmoja. Basi aliowaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe.
>
> Wakamwambia, jinsi gani basi Musa aliamura kumpa hati ya talaka, na kumwacha? Akawaambia, musa, kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu, aliwapa ruhusa kuwaumuhimuacha wake zenu, lakini tangu mwanzo haikuwa hivi.

1. Kulingana na Yesu, ni nini cha muhimu katika uhusiano wa ndoa?
2. Kwa nini sote hatuishi kulingana na umuhimu wa “mwili mmoja”.
3. Ni mifano gani mingine ya kuwa na, “ugumu wa mioyo”?

Yesu alisema kwamba umhimu wa Mungu ni kutopatikana katika mila za wanadamu, au katika barua ya Sheria, bali ni katika mpango ulioimarishwa “Kutoka Mwanzo”. Alisema kwamba Sheria inapinga umuhimu huu.Musa aliruhusu talaka kwa sababu ya “ugumu wa mioyo yetu” kuelekea mmoja na mwenzake.

# Hapo Mwanzo

## MWANZO 1:26-29

> 26 Mungu akasema, na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu, wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi.



© Carrie A. Miles, 2012

27 Mungu akamuumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu aliwaumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba.

28 Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia, zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi.

29 Mungu akasema, tazama nimewapa (neno nimewapa ni katika wingi) Kila mche utoao mbegu, ulio juu ya uso wa nchi yote pia, na kila mti ambao matunda yake yana mbegu, vitakuwa ndivyo chakuka chenu (chenu ni kwa wingi).

4. Ni nani aliyeumbwa kwa mfano wa Mungu, Mwanamume au Mwanamke?

5. Mungu anampa nani baraka ya kutiisha nchi, Mwanamume au kwa Mwanamke?

6. Mungu anampa nani baraka ya jukumu la kujaza nchi (watoto), Mwanamume au Mwanamke?

7. Gundua kwamba, kutiisha nchi na uwezo wa kuwa na watoto ulitolewa kama baraka sio amri. Hii ni kama kusema " Enda kwa amani"au "Ubarikiwe!" Je kugundua huku kwaweza kufanya mabadiliko kwa kufikiria kuhusu makusudi ya ndoa?

8. Je ni nini ambacho Mungu anampa Mwanamume na Mwanamke (kifungu 29)?

9. Tumejifunza nini hasa kuhusu mpango wa Mungu kwa uhusiano kati ya Mwanamume na Mwanamke? Katika vifungu hivi, je Mungu anahusika tofuti kati ya Mwanamume kwa Mwanamke?

Kila sehemu ya nchi iliyoumbwa amepewa Mwanamke kama vile alivyopewa Mwanamume.Huu ndio mpango wa Mungu kutoka mwanzo, mpango wake ulipofaulu, mungu akatangaza kwamba "ni chema sana" Hakusema hivyo wakati Mwanamume alipokuwa pekee yake. Lakini Mungu alisema kinyume, mungu alisema "si vema"huyo mtu awe pekee yake (Mwanzo 2). Hadi Mwanamke alipo simama karibu naye ndipo Mungu akaweka fimbo mikononi mwao na Katangaza kwamba kazi imekamilika, na njema sana (maneno haya yameongezwa na mwandishi Bushnell).

## Umejifunza nini / changamoto za kitamaduni.

10. Yesu aliwaambia mafarisayo kwamba umuhimu wa Mungu haungepatikana katika mila zao. Mwanzo1, inatuambia kuwa Mwanamke hatakiwi kuchukuliwa kama chombo tu, bali alipewa kila kitu sawa na Mwanamume. Tabia gani za kitamaduni ambazo haziendi sawasawa na umuhimu vile umeonyeshwa katika Mwanzo 1:26-29?

11. Je vifungu hivi vyaweza kukufanya ufikirie kuhusu uhusiano wako kwa njia tofauti?



© Carrie A. Miles, 2012

# SOMO LA 2 UHUSIANO WENYEWE

Katika somo la kwanza, tuliona kwamba Yesu alifundisha kwamba uhusiano wenyewe kati ya Mwanamume na Mwanamke haungepatikana katika mila ama katika sheria ya Musa.Lakini makusudi ya Mungu kwetu inapatikana katika jinsi alivyo tuumba.Katika Mwanzo 1, Mungu aliwaumba mwanamume na mwanamke kwa mfano wake, na akawapa wote jukumu la kutawala nchi na kuwakuza watoto.

Maandiko ya Kiebrania (Agano la Kale liliandikwa kwanza kwa Kiebrania) hutupa hasa tafsiri mbili kwa tukio moja.Mwanzo 1, hupeana “Picha Kubwa” ya kuumbwa. Mwanzo 2, hutupa “hutupa picha ndogo iliyofungwa” ya tafsiri ya tukio moja hilo, hapo ikitueleza kwa nini Mungu alituumba “Mwanamume na Mwanamke”.

## Kiumbe cha mapenzi (ngono)

### MWANZO 2:7, 18-25

7 Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai, mtu akawa nafsi hai.18 Bwana Mungu akasema, si vema huyo mtu awe pekee yake, nitamfanyia msaidizi wakufanana naye [Tafsiri ya Mfalme Yakobo: msaidizi wa kafanana naye]. 19 Bwana Mungu akafanyiza kutoka katika ardhi kila mnyama wa msituni, na kila ndege wa angani, Kamlate Adamu ili aone atawaitaje, kila kiumbe hai, jina lake. 20 Adamu akawapa majina yao kila mnyama wa kufugwa, na ndege wa angani, na kila mnyama wa mwituni, lakini hakuonekana wa kumsaidia Adamu aliyefanana naye. 21 Bwana Mungu akamletea Adamu usingizi mzito, naye akalala kisha akatwaa ubavu wake mmoja, akafunika nyama mahali pake, 22 na ule ubavu alioutwaa katika Adamu Bwana Mungu akaufanya mwanamke, akamleta kwa Adamu.

23 Adamu akasema, sasa huyu ni mfupa katika mifupa yangu na nyama katika nyama yangu, basi ataitwa mwanamke, kwa kuwa ametwaliwa katika mwanamume.

24 Kwa hivyo mwanamume atamwacha Baba yake na Mama yake ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja. 25 Nao walikuwa uchi wote wawili, adamu na Mkewe, wala hawakuona haya.



© Carrie A. Miles, 2012

## Msaidizi anayemfaa Mwanamume

1. Tukifwata kila tendo la uumbaji katika Mwanzo 1, mungu alitangaza kuwa alivyo viumba ni “vyema”. Je!kuna utofauti gani katika Mwanzo 2:18?

2. Mungu aliumba mtu na wanyama kutoka kwa ardhi ya nchi.Kuna utofauti gani kati ya kuumbwa kwa mwanamume na wanyama (msitari wa 7)?

3. Mwanamume hawezi kupata msaidizi anayefanana na wanyama, hii inatuambia nini kuhusu kile mwanamume anahitaji katika msaidizi wake? Mwanamke anafananaje na Mwanamume, wala sio wanyama?

Katika Kiebrania, maneno ambayo Mungu alitumia kumueleza msaidizi ambaye Mwanamume alihitaji ni “ezer kenegdo” Maneno haya yanatafsiriwa katika Kingereza kama “Msaidizi” au “Msaidizi mnayefanana”.

4. Watu huelewaje tamko la kusema Mwanamke aliumbwa awe msaidizi wa Mwanamume?

Shida ya kutafsri “ezer kenegdo” kama “msaidizi” inaonyesha kwamba mwanamke aliumbwa awe duni na awe chini ya mwanamume.Msaidizi anaonekana kama yuletunaweza kumwaajiri kufanya kazi mbaya ambazo hatuwezi kuzifanya sisi wenyewe, kama kuosha vyombo au kuchimba mashimo.Kuna neno katika Kiebrania linalotumika kumaanisha msaidizi wa chini au duni-an *eben***.** Lakini hili silo neno ambalo Mungu alitumia kuonyesha kile Mwanamume anahitaji.

> Badala yake, Mungu alisema mwanamume alihitaji “ezer kenegdo”.
>
> Neno ‘ezer, linapatikana mara 21 katika Agano la Kale.Linamaanisha “Msaidizi”…..mtu anayeweza kuwasaidia wenzake kwa mfano kuwasaidia au kuwapa msaada .Neno hili linapatikana mara mbili katika mwanzo 2. Mara 16 kutoka kwa 19 neno “ msaidizi” kumaanisha msaada kutoka kwa mtu aliye wa nguvu kukuliko wewe.Katika hali nyingi “msaada”ni Mungu mwenyewe ….Katika nafasi ambazo “ ezer” haihusiki kumaanisha Mungu, inatumika kwa watu kama Wafalme ambao huja kwa msaada wa mwingine…hakuna kadaicha? au kuweka chini kunakoshikamana na neno “msaada”. (Fleming)

Mfano wa kumaanisha neno “ezer” au “Msaada”Tazama Zaburi 46:1 “Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu, msaada utakaoonekana tele wakati wa mateso”.

Neno la pili “kenegdo”, linamaanisha “Kinachofaa au kinachofanana na Mwanamume.Neno hilo la Kihebrania linamaanisha “kuangaliana”Mungu alimaanisha Mwanamke awe ana kwa ana au kuwa kwa kiwango kimoja na Mwanamume.

> Kinacho wekewa mkazo ni utu wa kawaida na hali ya watu hawa wawili, pamoja na kulingana kwao. Musa alitumia neno hili katika kuandika kuwa kuumbwa kwa Mwanamke kwa sababu alitaka tuelewe kwamba Mungu alimfanya Mwanamke awe analingual na Mwanamume (Fleming, pp. 8-9).



© Carrie A. Miles, 2012

> “Wakati Mungu anaumba Hawa kutoka kwa ubavu wa Adamu, makusudi yake ni kwamba Hawa hatakuwa-sawa na wanyama “nguvu (au uwezo) wake utalingana na uwezo wa mume wake” (Freedman).

Mungu aliumba mwanamke awe mtu wa nguvu kabisa- kiroho, kiakili, na kimsisimko - kumsaidia mwanamume kubeba mizigo. Kama wa kulingana naye angeweza kutoa msaada anaohitaji.

Kumpata huyu msaidizi kulingana na mwanamume, ilimbidi Mungu amtoe kutoka kwa mwili wa mwanamume mwenyewe. Mungu akamletea mwanamume usingizi mzito, na kutwa sehemu ya upande wake(tafsiri yenu inaweza sema “ubavu” lakini likuta kipande kikubwa cha upande wake, sio tu mfupa mdogo mmoja)na kuumba mwanamke kutoka kwa ubavu huo.(vifungu 21,22)

5. Mwanamume anasema nini anapomwona Mwanamke kwa mara yake ya kwanza?(kifungu 23) Je! Unasikia furaha katika maneno haya?

6. Kutoka kwa maneno hayo, je!unafikiria kwamba wazo la mwanamume la “msaidizi wa kunifaa”angeweza kuwa mjakazi wa nyumba au mtu wa pekee? (spesheli?)

> Watu wa mila na utamaduni mara kwa mara wanapingana kwamba kupeana jina la mwanamke katika kifungu cha 23 ni kukiri kwa Adamu kumtawala mkewe.Lakini “mke”siyo jina kamili na kile Adamu anasema hakifwatii hali ya kupewa jina. “Mke”[ishshah] inamaanisha hali ya uke na hali ya uume ya “mume”ni [ish].Walishiriki jina na kila kitu wakati huu. Kile Adamu anasema katika Katangese kwa furaha ni “Hapa[mwishowe!] ni mtu kama mimi! (Fleming).
>
> Only after the creation of the wamen was the earth creature referred to as a man!

## Umejifunza nini/ Changa moto za kitamaduni.

7. Kasisi Daktari Tonny Baucum anasema kuwa Mungu hakumuumba mwanamke kumkamilisha mume, bali kukamilisha mfano wa Mungu.Maneno haya yanamaanisha nini kwako?

8. Utaonyeshaje heshima kwa mwanamke kiumbe cha Mungu awe “Msaidizi wa kafanana” Mwanamume badala ya “Msaidizi wa”au “Msaidizi” kwa Mwanamume?

9. Msitari wa 24 unasema “kwa hiyo mwanamume atamwacha Baba yake na Mama yake naye ataambatana na mkewe , nao watakuwa mwili mmoja”Yesu alisema kuwa ni Muumba ndiye aliyeyasema haya mwenyewe( Mathayo Mtakatifu 19:4-5)Hii inamaanisha nini kuhusu heshima ya mwanamume itategemea-kwa wazazi wake au kwa mwanamkewe?Je hawa wachumba wataheshimuje wazazi wao huku wakiwa bado wanatoa heshima zao kwa kila mmoja wao?

10. Je wazazi watawasaidiaje watoto wao walioona msaada wao kwanza wa kutoa heshima kwa Bwana wao au Mke wao?

11. Kifungu cha 25 “kinasema, nao walikuwa uchi wote wawili Adamu na Mkewe wala hawakuona haya” kuwa uchi ni hali ya kawaida ya mwilini, aibu au kukosa aibu in hali ya msisimko, au kiroho.inamaanisha nini uhusiano “kuwa uchi wala hawakuona aibu”?



© Carrie A. Miles, 2012

# SOMO LA 3 NAFASI YA MUME NA MKE KWA MUNGU

Mungu alituumba tutunze bustani nzuri ambamo mahitaji yetu yote yanapatikana. Mwanzo 3 Inatuonyesha kwamba kwa sababu ya tama ya mwanadamu kufanya vitu kwa njia yetu, tunaishi maisha ya uhitahi na "jasho"au "maumivu"kufanya kazi badala yake. Maumivu haya si matakwa ya mungu kwetu. Somo hili linatuonyesha kama ilivyo sasa vile ilivyo kuwa mwanzo, mungu hupenda vitu vizuri kwetu.

## Kutokutii

### MWANZO 3:1-13

1 Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliyefanya
Mungu.Akamwambia mwanamke, ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, msile
matunda yote ya miti ya bustani? 2 Mwanamke akamwambia nyoka, matunda ya miti
ya bustani twaweza kula, 3 lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu
amesema, Msiyale wala msiyaguze, msije mkafa, 4 Nyoka akamwambia mwanamke,
hakika hamtakufa, 5 Kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula
matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho nanyi mtakuwa kama Mungu mkijua
mema na mabaya.6 Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwa chakula,
wapendeza macho, nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa, basi alitwaa katika
matunda yake akala, akampa na mumewe[aliyekuwa naye]naye akala.7
Wakafumbuliwa macho wote wawili wakajijua kuwa wa uchi, wakashona majani ya
mtini, wakajifanyia nguo,

8 Kisha wakasikia sauti ya Bwana Mungu, akitembea katika bustani wakati wa
jua kupunga, Adamu na mkewe wakajificha kati ya miti ya bustani, bwana Mungu
asiwaone,9 Bwana Mungu akamwita Adamu akamwambia uko wapi?10 Akasema,
nilisikia sauti yako bustanini, nikaogopa kwa kuwa mimi ni uchi,
nikajificha.11Akasema, ni nani aliyekwambia ya kuwa u uchi? Je!Umekula wewe
matundaya mti niliokuagiza usiyale?12 Adamu akasema, huyu Mwanamke uliyenipa
awe pamoja nami ndiye aliyenipa matunda ya mti huo, nikala.13 Bwana Mungu
akamwambia Mwanamke, nini hili ulilolifanya? Mwanamke akasema, nyoka
alinidanganya, nikala.



© Carrie A. Miles, 2012

1. Ni nani wote walikuwako wakati nyoka anazungumza na mwanamke (kifungu 6) (Gundua mfano wa maneno yaliyotumika katika mlango huu wote ni kwa wingi, hiyo ni kusema, wakati nyoka anasema “msiyale, mtakapokula”anazungumzia mtu zaidi ya mmoja.)

2. Ni nini kilifanyika kwa Mwanamume na Mwanamke wa kwanza kwa uhusiuno wao wakati walifanya dhambi?Ni nini kilifanyika kwa uhusiano wao na Mungu?

## MWANZO 3: 14-24

14 Bwana Mungu akamwambia nyoka, kwa sababu umefanya hayo, umelaaniwa wewe kulikowanyama wote, na kuliko hayawani wote, walioko mwituni, kwa tumbo utakwenda, na mavumbi utakula siku zote za maisha yako,15 nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino.

16 Akamwambia mwanamke [Bwana Mungu], hakika nitakuzidishia uchungu (neno hili uchungu, linaweza kutafsiriwa kama, kazi ya uchungu, au kufanya kazi kwa uchungu) wako, na kuzaa kwako, kwa uchungu utazaa watoto, na tamaa yako itakuwa kwa mumeo, naye atakutawala.

17 Akamwambia Adamu, kwa kuwa umeisikiliza sauti ya mke wako, ukala matunda ya mti ambao nilikuagiza nikisema, usiyale, ardhi imelaaniwa kwa ajili yako, kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako, 18 michongoma na miiba itakuzalia, nawe utakula mboga za kondeni, 19 kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa, kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi.

20 Adamu akamwita mkewe jina lake Hawa, kwa kuwa yeye ndiye aliye mama yao wote walio hai.



© Carrie A. Miles, 2012

3. Mwanzo 3:14-19 mara nyingi husemwa kuwa ni “laana”Angalia kwa uangalifu katika hivyo vifungu.Mungu alitumia neno “imelaaniwa au umelaaniwa” mara mbili. Ni nini kililaaniwa?

Mungu aliweka laana kwa ardhi, lakini hakulaani Mwanamume au Mwanamke. Badala yake kile Mungu anawaambia katika Mwanzo 3:14-19 ni unabii wa kile kingetendeka kwao kwa kile walichokifanya. Haya mambo mabaya ni matokeo ya matendo yao waliyoyatenda.

4. Kuelewa tafauti ulio kati ya laana kinyume cha unabii wa matokeo ya tabia fulani, fikiria kuhusu mtoto mdogo anayeweka mkono wake kwa moto.Baba yake akasema Hapana!Hapana!usiguze moto, utaungua.Mtoto huyu akakataa kusikia sauti ya Baba yake akaungua na akaumia.Je! Mtoto huyu anaumia kwa sababu Baba yake alimlaani?

Mahali pengine maandiko yanatuonyesha kuwa mtu au Kirundi cha watu wanaweza kulaaniwa.Lakini kusoma kwa uangalifu Mwanzo 3 inatuonyesha kuwa Mungu hakuweka

5. Hata vile Mungu anavyoonyesha, uchungu na kung’ang’ana kwa Mwanamume na Mwanamke watakaopata pasipo yeye, mungu anatuhakikishia kuwa hajatuacha kabisa.Jadiliana tumaini ambalo Mungu alitupa katika Mwanzo 3:15.

## Umejifunza nini/Changamoto za kitamaduni

6. Watu wengi wamefundishwa kwamba Mwanamume na Mwanamke walilaaniwa na Mungu katika Mwanzo 3.Je unaelewaje Mwanzo 3:16-19 kama unabii, au maelezo ya Mungu kuhusu matokeo ya tabia zao (sio laana) inaweza kugeuzaje jinsi unavyo fikiria kuhusu nafasi ya Mwanamume na Mwanamke kwa Mungu?

7. Je! Ni mambo gani ya kawaida yaliyo tofauti katika njia hii ya kuelewa laana kwa ardhi sio kwa watu?



© Carrie A. Miles, 2012

# SOMO LA 4 MWISHO WA UMOJA

Neno la mwisho katika Mwanzo 2. Linaonyesha kwamba Mwanamume na Mwanamke "walikuwa uchi wala hawakuona haya". Uhusiano kama huo ambao kila mmoja wao ni salama na wazi, inabidi uimarishwe katika Mungu, kama ilivyo kuwa katika kuumbwa. Sasa katika Mwanzo 3, tunaona kile kinachoweza kufanyika tunapokataa Mungu katika uhusiano wetu.

## Kutengana

### MWANZO 3:1-7, 16-24

1 Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliyefanya
Mungu.Akamwambia mwanamke, ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, msile
matunda yote ya miti ya bustani? 2 Mwanamke akamwambia nyoka, matunda ya miti
ya bustani twaweza kula, 3 lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu
amesema, Msiyale wala msiyaguze, msije mkafa, 4 Nyoka akamwambia mwanamke,
hakika hamtakufa, 5 Kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula
matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho nanyi mtakuwa kama Mungu mkijua
mema na mabaya.6 Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwa chakula,
wapendeza macho, nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa, basi alitwaa katika
matunda yake akala, akampa na mumewe [aliyekuwa naye] naye akala.7
Wakafumbuliwa macho wote wawili wakajijua kuwa wa uchi, wakashona majani ya
mtini, wakajifanyia nguo,

16 Akamwambia mwanamke[ Bwana Mungu], hakika nitakuzidishia uchungu(neno hili uchungu, linaweza kutafsiriwa kama, kazi ya uchungu, au kufanya kazi kwa uchungu) wako, na kuzaa kwako, kwa uchungu utazaa watoto, na tamaa yako itakuwa kwa mumeo, naye atakutawala.

17 Akamwambia Adamu, kwa kuwa umeisikiliza sauti ya mke wako, ukala matunda ya mti ambao nilikuagiza nikisema, usiyale,



© Carrie A. Miles, 2012

ardhi imelaaniwa kwa ajili yako, kwa uchungu utakula mazao yakesiku zote za maisha yako,18 michongoma na miiba itakuzalia, nawe utakula mboga za kondeni,19 kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa, kwa maana u mavumbi wewe,  nawe mavumbini utarudi.

20Adamu akamwita mkewe jina lake Hawa, kwa kuwa yeye ndiye aliye mama yao wote walio hai.

## From the Garden of Eden to a World of Thorns

Kutoka kwa bustani kwenda kwa ulimwengu wa miiba. Kama vile Mungu alivyoumba, wachumba hawa wawili walifurahia umuhimu wa uhusiano wao, pamoja na uhusiano wao na Mungu, na uhusiano wao na viumbe vyote.Waliishi katika bustani iliyowapatia mahitaji yao yote.

Dhambi iliwalazimisha watoke kwenye bustani na kuingia katika ulimwengu wa miiba na michongoma.Badala ya kufurahia maisha ya kutunza bustani nzuri, mwanamume na mwanamke lazima kujitosheleza katika maisha ya mahitaji na hofu.

Wakulima wanahitaji watoto wengi ili wawasaidie katika kung'ang'ana ili wapate chakula cha kuwatosha na kuwatunza wakati ni wagonjwa ama wakiwa wazee.Katika umasikini, kazi ya muhimu sana kwa wanawake ni kuzaa watoto.Adamu alikiri ukweli huu baada ya anguko, alisema kwamba, mke wake ataitwa  "Hawa"kwa sababu atakuwa mama wa wote walio hai.(Kifungu cha 20)

Kama vile Mungu alivyotabiri, katika ulimwengu wa  anguko, wanawake lazima wafanye zaidi ya kuzaa watoto tu. Ijapokuwa tafsiri nyingi za Biblia hutafsiri sehemu ya kwanza ya 3:16 kama "nitakuzidishia uchungu wako, katika kuzaa watoto" tafsiri nzuri ni "Hakika nitakuzidishia uchungu wako(au kazi ya jasho yako) na kuzaa kwako, kwa uchungu utazaa watoto" (Flemings). Adamu na Hawa wanaambiwa kwamba watakumbana na "uchungu", au "uchungu"na kazi ya jasho kama matokeo ya kugeuka kwao kwa Mungu.Hawa atafanya kazi kwa uchungu na kwa jasho ili aweze kula kama Adamu pia.

Kazi ya wanawake ya kuzaa watoto huwafungia kwenye nyumba na kazi ya wanaume sio kama hiyo ya wanawake.Kazi nyingine ni ngumu kufanya wakati mwanamke ana mimba(mja mzito) au ananyonyesha mtoto mdogo.Tamaduni zote zimejifunza kugawanya kazi ili mwanamke afanye kazi inayoweza kufanywa bila kumpoteza mtoto wake.Kazi ya wanaume ni ile iliyobaki, yani kazi ambayo akina mama Hawaiwezi kuifanya.Kile kinachochukuliwa kuwa kazi ya wanaume kinyume cha kazi ya wanawake hubadilika kulingana na hali.Kwa mfano, ikiwa mtu anaweza kushika samaki kwa urahisi kwa kuweka wavu katika maji karibu na nyumbani, wanawake wangefanya uvuvi.Ikiwa kushika samaki kunahitaji mvuvi aende kwenye bahari kwa meli akitumia siku nyingi kwa wakati mmoja, wanaume watavua samaki.



© Carrie A. Miles, 2012

Kihistoria, majukumu ambayo yalihitaji watu wengi kufanya kazi pamoja, yalifanywa "kazi za wanaume"Wanaume hupanda vyakula, kwa mfano, ni "wanaume"kwa sababu wanaume wana mvuto kupita nyuma zao, wanaweza kuwakusanya wafanyakazi wengi, wake wao, watoto, wanaowategemea, wanatakiwa kupanda vyakula na kuvuna vyakula na kuvileta sokoni (Guyer).

1. Ni kazi gani katika mila na desturi zenu husemwa kuwa ndio kazi ya mwanamke? Wanaume hufanya kazi gani? (Gundua katika nyakati za kisasa, kazi ambazo wanaume walikuwa wakifanya siku baada ya siku, kama kutengeneza shamba, kujenga nyumba, wengi wao hawafanyi kazi hizo leo.Ungetaka kujua jinzi mambo yalikuwa hapo zamani ukijibu swali hili).

## Watawala

Mwanamke wa nyumbani ana kazi nyingi, inamaanisha kazi nyingi nje ya nyumbani mwake si kazi yake.Hii husababisha wanaume kuwatawala wanawake katika soko, kanisani, kwenye vyama, kwenye serikali na katikaFamilia. Kwa sababu wanaume wanahusika na kazi zinazo hitaji ushirikiano na watu wengi, wanajipata kwamba inawabidi wawatawale wengine au watawaliwe na wengine.

Uchumi ukizorota, watu wachache wanabaki wakiwa juu ya wengine na watu wengi wanabaki kuwa chini yao.Neno hili Watangulizi au watawala lilitumika kuonyesha hali ya nguvu katika ulimwengu wa anguko, utangulizi humaanisha tu utawala wa wanaumejuu ya wanawake bali utawala wa watu wachache juu ya kila mmoja, wanaume na wanawake.Hali ya wanaume kutawala wanawake na watu wachache, wakubwa kutawala wenzao ni matokeo ya anguko.

Katika Mwanzo 1:28, mungu aliwabariki mwanamume pamoja na mwanamke na watoto kutawala na kutiisha nchi yote.Baada ya anguko umoja huu wa kiungu uligawanyika vipande.Vitu vilivyotolewa bure kama baraka vikawa vigumu kuvipata.Uwezo wa kuzaa watoto ulikusudiwa na Mungu kama baraka, sio kumzuia na kumpa vizuizi katika maisha yake.Baraka ya kutawala na kuitiisha nchi ikawa uzito wa mwanamume vile anavyong'ang'ana kutawala, sio kutawala nchi pekee yake bali kutawala watu wengine pia.

## Anguko la Wanaume

2. Je! Mungu alisema kwamba ni nini kingefanyika kwa mwamume kwa sababu ya dhambi(msitari wa 17-19)?

| **Mwanzo 3** | **Ukweli wa nchi ya anguko** |
|---|---|
| Mwanamume atafanya kazi ngumu | Wanaume lazima wafanye Kazi kwa bidii ili wawe salama. Mfano: |
| Mwanamume atakula Kwa jasho lake | Kusumbukana, kutaka, kushindana, kulazimishwa kuwa bora zaidi, kutokuonyesha udhaifu, kutawala wengine. Mfano: |
| Watarudi kwa ardhi | Mauti |

3. Je wanaume kungang'ania heshima, au nguvu juu ya wengine kunachangiaje utamaduni wenu? Ndoa? Makanisa?



© Carrie A. Miles, 2012

## Anguko la Wanawake

4. Mchoro wa chini unaorodhesha vitu ambavyo Mungu alisema vitafanyika kwa mwanamke katika ulimwengu wa anguko (kifungu cha 16) toa mfano jinsi wanawake huumia kwa sababu ya matokeo ya mwanguko katika maisha yao leo?

| **Mwanzo 3** | **Ukweli wa nchi ya anguko** |
|---|---|
| Mwanamke kuzaa watoto kwa uchungu | Umuhimu wa wanawake kuzaa watoto.<br>Watoto ni mhimu kutumikia wazazi wao, sio kujitumikia wao wenyewe.<br>Wachumba satiatewatoto wengi kuliko jinsi wanavyoweza kuwatunza.<br>Matakwa ya kuwa na watoto wengi huchangia kuoa wake wengi na kulipisha mahari. Mfano: |
| Mwanamke atafanya kazi kwa uchungu | Mwanamke lazima afanye kazi kwa nguvu ili awe salama.<br>Kupata watoto kwa uchungu, mwanamke kuzuiliwa kufanya kazi ambazo watoto wangefanya Waikato. Mfano: |
| Tamaa ya mwanamke ni kwa mume wake. | Wanawake wanawategemea waume wao kifedha.<br>Wanawake hupenda waoleke kwa wanaume wenye nguvu, wenye utawala. Mfano: |
| Wanaume watawatawala wanawake | Wanaume watatawala taasisi mbali mbali.<br>Wanaume Watakuwa na nguvu nyingi katika uhusiano wa ndoa.<br>Wanawake kuwa chini ya wanaume. Mfano: |

## Umejifunza nini/Changamoto za kitamaduni

5. Somo hili hutueleza kwamba uwezo wa wanaume na msukumo wa kuwatawala wenzao, wake wao na watoto wao katika maisha yao ni matokeo ya dhambi sio makusudi ya Mungu katika uumbaji.Gundua tabia ambazo sharti zibadilishwe ili kushinda matokeo ya dhambi katika maisha yetu.

Katika masomo yajayo, tutaona jinzi mafundisho ya Yesu na Paulo huondoa laana kutoka kwa ardhi na kurejesha Mume na Mke kwa uhusiano kamili ambao Mungu aliwaumbia.



© Carrie A. Miles, 2012

# SOMO LA 5 UKOMBOZI KUTOKA KWA LAANA

Wakati mwanamume na mwanamke wa kwanza walipokataa makusudi ya Mungu katika maisha yao (Mwanzo 3), uhusiano wa Mungu wa kwanza na mume na mke ukaharibika. Tunafanya "kazi kwa jasho" ili tuweze kuishi.Ndoa haikuhusika na umoja na upendo ambao tuliumbiwa, ndoa ikigeuka kuwa chombo cha kupigana kinyume cha ardhi. Wanawake hufanya kazi kubwa kwa kuzaa watoto, na kuwatunza na kutunza bwana zao. Kazi hii nzito katika maboma yao huwafanya wawategemee wanaume wao kwa pesa na kwa ulinzi. Wanaume wana wasiwasi ya kushindana kupata nguvu dhidi ya wanaume wenzao. Ni vigumu kufikia umuhimu wa kuumbwa "mwili mmoja, uchi wala hawakuona haya"-katika ulimwengu kama huu.

Maisha ya Yesu na mafundisho yake yanatuonyesha njia ya kurudi kutoka kwa uchungu na shauku turudi kwa maisha ya bustani ambayo tuliumbwa kwayo.

## MATHAYO MTAKATIFU 19:16-25

Na tazama, mtu mmoja akamwendea akamwambia, Mwalimu, nitende jambo gani jema ili nipate uzima wa milele? Akamwambia kwani kuniuliza habari ya wema ? Aliye mwema ni mmoja. Lakini ukitaka kuingia katika uzima, zishike amri. Akamwambia zipi? Yesu akasema, ni hizi, usiue, usizini, usiibe, usishuhudie uwongo, waheshimu baba yako na mama yako, na, mpende jirani yako kama nafsi yako. Yule kijana akamwambia, haya yote nimeyashika, nimepungukiwa na nini tena? Yesu akamwambia, ukitaka kuwa mkamilifu, enenda ukauze ulivyo navyo, uwape masikini, nawe utakuwa na hazina mbinguni, kisha njoo unifuate. Yule kijana aliposikia neno lile akaenda zake kwa huzuni, kwa sababu alikuwa na mali nyingi.

Yesu akawambia wanafunzi wake, Amin, nawambieni ya kwamba itakuwa shida tajiri kuingia katika ufalme wa mbinguni. Nawambia tena, ni rahisi zaidi ngamia kupenya tundu ya shindano, kuliko tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu. Wanafunzi waliposikia, walishangaa mno, wakisema, ni nani basi awezaye kuokoka? Yesu akawakazia macho, akawambia, kwa wanadamu hilo haliwezekani, bali kwa Mungu yote yawezekana.



© Carrie A. Miles, 2012

1. Ni tabia gani inahitajika kutoka kwa mtu mkubwa, yule aliyefaulu, au aliye wa cheo kikubwa katika hali ya ulimwengu? Hii humletea majukumu na shauku gani kwa mtu huyo? Kwa wale wanao jaribu kuwa watu wa muhimu?

2. Wanafunzi wa Yesu wanashangaa kwa kile alisema kuhusu tajiri. Ni kiwango gani ambacho wakristo wanashiriki kuamini kwamba tajiri wanastahili kuliko masikini?

## MATHAYO MTAKATIFU 6:25-34

> Kwa sababu hiyo nawaambieni, msisumbukie maisha yenu, mle nini au mnywe nini, wala miili yenu, mvae nini, maisha je!si zaidi ya chakula, na mwili zaidi ya mavazi?Waangalieni ndege wa angani, ya kwamba hawapandi, wala hawavuni, wala hawakusanyi ghalani, na Baba wenu wa mbinguni huwalisha hao.Ninyi je! Si bora kuliko hao?Ni yupi kwenu ambaye akijisumbua aweza kujiongeza kimo chake hata mkono mmoja?Na mavazi ni ya nini kuyasumbukia?Fikirini maua ya mashamba, jinsi yameavyo, hayafanyi kazi, wala hayasokoti nami nawaambia, ya kwamba hata sulemani katika fahari yake yote hakuvikwa vizuri kama mojawapo la hayo. Basi, ikiwa Mungu huyavika hivi majani ya kondeni, yaliyopo leo, na kesho hutupwa kalibuni, je!Hatazidi sana kuwavika ninyi, enyi wa imani haba?Msisumbuke, basi, mkisema, tule nini?Au Tuvae nini?Kwa maana hayo yote Mataifa huyatafuta, kwa sababu Baba yenu wa mbinguni anajua ya kuwa manahitaji hayo yote. Bali utafuteni kwanza ufalme wake na haki yake na hayo yote mtazidishiwa.
>
> Basi msisumbukie ya kesho, kwa kuwa kesho itajisumbukia yenyewe.Yatosha kwa siku maovu yake.

3. Tondoo gani ambayo Yesu anaifanya katika sehemu hii?

4. Linganisha maneno ya Yesu na neno la Mungu kwa Adamu katika Mwanzo 3:17-19

## MWANZO 3:17-19

> Ardhi imelaaniwa kwa ajili yako, kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako, michongoma na miiba itakuzalia, nawe utakula mboga za kondeni, kwa jasho la uso wako utakula chakula hata utakaporudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa, kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi.



© Carrie A. Miles, 2012

Katika sehemu nyingi Yesu aliwahakikishia wanaomfuata kwamba wamerudi katika utele. Badala ya miiba, wale wanao mrudia Mungu wanaweza kutarajia maisha ya maua.

Hii haimanishi ya kwamba hatuhitaji kufanya kazi kupata hivi vitu. 2Wathesolanike 3:6-10, inasema……. Jitengeni nafsi zenu na kila ndugu aendaye bila utaratibu,……bali kwa taabu na masumbufu, usiku na mchana tulitenda kazi,…….lakini kwa makusudi tufanye nafsi zetu kuwa kielelezo kwenu, mtufuate.Kwa kuwa hata wakati ule tulipokuwapo kwenu tuliwaagiza neno hili, kwamba ikiwa mtu hataki kufanya kazi, basi, asile chakula.

Katika uumbaji, Mungu alifanya binadamu kutunza, kulinda bustani (Mwanzo 2:15). Kwa anguko, ardhi ililaaniwa na mume na mke wote wanalazimishwa kufanya kazi ngumu na ya uchungu. Tunapomkubali Kristo, hutukomboa, kutununua kutoka kwa utumwa wa ardhi. Tukiishi katika imani, tutatoka kwenye utumwa wa uchungu, kutoka kwenye uovu au ulafi (Mwanzo 3:16-17) turudie kutunza kwa furaha au kulinda bustani. Hatusitahili kuwa na hofu kwa vitu kama; vyakula, nguo, muda gani tutaishi-------na kadhalika.

5. Tazama vifungu hivi (kama unafanya katika kikundi, kila mtu achukue kifungu) anguko lipi ambalo Yesu anabadilisha katika kila kifungu?

1Wakorintho 15:22, 26

Timotheo 2, 1:10

Ufunuo wa Yohana 7:16, 17

Ufunuo wa Yohana 21:3-4, 22:2-3.

Ufunuo wa Yohana 22:2-3

## Umejifunza nini?

6. Kuna utofauti gani iliopo kati ya “kufanya kazi kwa jasho”, na “kutunza” au “kulinda” bustani? Je! Kuna mifano ya maneno haya katika maisha yako?

7. Je! Vitu ambavyo Yesu alituahidi ni vya mbinguni tu? Kama inatubidi tuwe na ufalme wa mbinguni sasa, katika maisha haya, je hii inadhuru vipi njia tunayoishi?

8. Je! Kuwa mkristo inamaanisha kuwa mtu hasitahili kufanya kazi? Au kazi hiyo ni ya chini ya mkiristo?

9. Kama umekombolewa na unaona kazi kama “kutunza bustani” badala ya “kufanya kazi kwa jasho” hiyo itadhuru kwa namna gani jinsi unavyo wachukua wanaume / wanawake? au watoto wako?



© Carrie A. Miles, 2012

# SOMO LA 6 HESHIMA UTAWALA NA KUTIISHA

Utawala hufikiriwa kuwa wanaume hujaribu kuweka wanawake wao katika nafasi ya chini na wanaume kwa nafasi ya juu.Mwana Historia wa Agano Jipya bwana S.Scott Bartchy anasema,hatahivyo,Gundua kwamba utawala si kwamba wanawake kuwa chini ya wanaumme bali utawala wa watu wachache juu ya kila mmoja,mke au mume.Kung’ang’ana huku kwa nguvu kati ya wanaume huleta aina ya utumwa,uajiri/uhusiano wa kiimla na uhusiano wa kimabavu au wa lazima.Katika utamaduni wa utawala,ambao huitwa kama heshima/utamaduni wa aibu,wanaume wanang’ang’ania na kupigania heshima,nguvu,utukufu na cheo cha juu,juu ya wenzake.Mtu akidumisha kiburi chake na kuzuia kuangushwa ni mambo makuu ya muhimu.Matusi yote kwake lazima yalipishwe kisasi,kwa kuwa kutokulipisha kisasi kila tusi kunaweza kuondoa heshima kwa familia yake na anaweza kuonenkana mdhaifu.Vita,ugomvi wa kikabila,uharibifu na kufanya vitu kwa kimabavu ni mambo ya kawaida kwa vikundi vya jamii Viking’ang’ania usalama wao kati ya mapato yasiyotosheleza.Wanaume inawalazimisha kuonyesha uume wao au nguvu katika kunywa pombe nyingi, kulala na wanawake wengi,kupata watoto kutoka kwa wanawake wengi,au kudharau wanaume wengine.Njia moja ya kuchokoza wanaume wengine ni kutongoza au kunajisi mwanamke katika familia yake,jambo linalowafanya wanawake kuwa na hatari.Msukumo wa ulimwengu wa kupata faida ya sifa ya mtu,kulipiza kisasi matusi,na kumzuia aibu,husababisha mtu awe na hamu kubwa ya kutaka Wana ambaowanaweza kumsaidia Baba yao au familia yake ifikie nafasi ya juu.

Katika wakati wa Kristo, ulimwengu uliojulikana uliongozwa na warumi.Utamaduni wa Kirumi na wa Kiyahudi ulikuwa wa utawala.(Ijapokuwa sheria ya Agano la Kale ilisaidia kumzuia uhalifu kati ya Wayahudi.)Yesu alifundisha wasikilizaji wa Kiyahudi, Mtume Paulo aliwaandikia watu waliokuwa wakiishi katika miji ya Kirumi.

## Heshima ya Kibinadamu

### MATHAYO MTAKATIFU 5:38-41

> 38 Mmesikia kwamba imenenwa,jicho kwa jicho,na jino kwa jino, 39 Lakini mimi nawaambia, msishindane na mtu mwovu,lakini mtu akupigaye shavu la kuume, mgeuzie na la pili. 40 Na mtu atakaye kukushitaki na kuitwaa kanzu yako, mwachie na joho pia. 41Na mtu atakaye kulazimisha mwendo wa maili moja, nenda naye mbili.

Yesu hakusema kuwa mtu haimpasi kujitetea kinyume cha valise wa kimabavu.Tendo alilosema kuhusu kupigwa shavu ni kukushitaki kwa uongo kulazimishwa kazi,ni matusi,sio vitisho vya kawaida.Heshima/aibu ya utamaduni inasisitiza mtu akikuchokoza kwa vyovyote lazima ulipishe kisasi au mtu na familia itakosa mwelekeo.Yesu alifundisha kinyume cha mvuringon wa utamaduni wa heshima na aibu.Ukitukanwa,Yesu alisema, uyaache matusi hayo hapo hapo. Paulo pia aliandika vivyo hivyo kwamba wakristo ambao wanatafuta kulipiza kisasi kwa wakristo wengine tayari wameshindwa. “Basi imekuwa upungufu kwenu kabisa kwamba mnashitakiana ninyi kwa ninyi.Maana si afadhali kudhulumiwa? Maana si afadhali kunyang’anywa mali zenu” (1Wakorintho 6:7).



© Carrie A. Miles, 2012

1. Kuna shida gani ukisisitiza kwa kulipiza kisasi? Je! Kubishana huku kuna mwisho?

## Utawala

### LUKA MTAKATIFU 9: 59-60.

Akamwambia mwingine,Nifuateni.Akasema Bwana nipe ruhusa kwanza niende nikamzike baba yangu 60 Akamwambia waache wafu wawazike wafu wao,bali wewe enenda ukautangaze ufalme wa Mungu.

2. Je!Yesu alikuwa anampa nini huyu kijana?

Kulingana na majibu ya ukali ya Yesu,Bartchy anachangia kuwa baba wa huyu kijana hakuwa amekufa! Kijana alikuwa anasema kwamba, kabla ya kumfuata Yesu,Kijana huyu alitaka aende nyumbani amtumikie baba yake hadi afe ndipo angemfwata Yesu.Katika nyakati hizi akina baba walitawala familia zao kabisa na wanaume waliotaka urithi wao,iliwabidi waheshimu baba zao wakati wote baba zao wakiwa hai.

Hapa Yesu alishutumu utawala wa wafu,utamaduni wa mali huwaambia watu kutafuta vitu vya dunia badala ya vitu vya Ufalme wa Mungu.Katika njia iyo hiyo kijana alifikiri kuwa atatekeleza jukumu kulingana na desturi na utamaduni wake. Kwa mfano , " Zika baba yake"na kuchukuwa urithi wake-na atoroke kuwa kama baba yake anavyotaka hapo mwishowe.Hatuwezi kumdanganya shetani,tukiishi kwa sheria za ulimwengu,tutakufa kwa sheria hizo.

3. Kama huku ndiko kuelewa vizuri maandiko haya,ni akina nani ndio wafu ambao Yesu anamaanisha.Yesu alimaanisha nini aliposema,"Waache wafu wawazike wafu wao"?

## Kiburi na Nguvu

### MARKO MTAKATIFU 10:35-37

17.

35. Na Yakobo na Yohana, wana wa Zebedayo, wakamwendea wakamwambia ,mwalimu, twataka utufanyie lo lote tutakalo kuambia 36 Akawaambia mwataka niwafanyie nini? 37 Wakamwambia utujalie sisi tuketi mmoja mkono wako wa kuume,na mmoja mkono wako wa kushoto,katika utukufu wako.

4. Je! Yakobo na Yohana walikuwa wanauliza nini?



© Carrie A. Miles, 2012

## ENDELEA NA MARKO MTAKATIFU 10:41-45.

41. Hata wale kumi (Mitume wengine) waliposikia wakaanza kuwakasirikia Yakobo na Yohana.42. Yesu akawaita akawaambia, mwajua ya kuwa wale wanaohesabiwa kuwa wakuu wa mataifa huwatawala kwa nguvu,na wakubwa wao huwatumikisha.43. Lakini haitakuwa hivyo kwenu,bali mtu anayetaka kuwa mkuu kwenu,atakuwa mtumishi wenu, 44. Na mtu anayetaka kuwa wa kwanza wenu atakuwa mtumwa wa wote.45. Kwa maana Mwana wa Adamu naye hakuja kutumikiwa bali kutumika,na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi.

5. Kwa nini Mitume wengine kumi waliwakasirikia Yohana na Yakobo?

6. Yesu aliwaambia nini akiwajibu?

Maneno hayo ya kushangaza yalileta swali kwa wanafunzi wa Yesu, kulingana na aina ya nguvu zinazofanya kazi katika "utukufu wake"kwa kuleta wazo la kinyume ya matarajio ya kawaida yanayoambatana na cheo cha " Mwana wa Adamu"Kulingana na Danieli 7:13-14, Yule "aliye kama Mwana wa Adamu"aliyechukuliwa katika karne yao kabla ya Yesu kama anayekuja kuhukumu ulimwengu, "atapewa utawala na utukufu na ufalme, kwamba watu wote, mataifa, lugha, watamtumikia".Yesu alijitambulisha kuwa Mwana wa Adamu, na akakataa mambo yanayoambatana na jukumu la cheo chake ila yeye akawa tayari kutumikia wengine hata kwa gharama ya maisha yake (Bartchy,1987)

# Kushindana kwa Kikabila

## LUKA MTAKATIFU 10:25-39

Na tazama Mwana- sheria mmoja, alisimama akamjaribu,akasema, "Mwalimu" "nifanye nini ili niurithi uzima wa milele"? " Akamwambia imeandikwa nini katika torati"?…Akajibu akasema, " Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote,na kwa roho yako yote,na kwa nguvu zako zote,na kwa akili zako zote, na jirani yako kama nafsi yako".Akamwambia "Umejibu vema,fanya hivi nawe utaishi".

Naye akitaka kujidai haki,alimwuliza Yesu,"Na jirani yangu ni nani"?



© Carrie A. Miles, 2012

Gundua,hapa katika utangulizi wa hadithi ya msamaria mwema kwamba mwanasheria alisimama “amjaribu” Yesu.Unaposoma Injili,gundua kwamba kila wakati mtu alikuja kumjaribu yeye.Hii ni seheme ya heshima/utamaduni wa aibu,ambako watu wanajumuika katika mashindano ya maneno kujaribu kumwaibisha mwenzao au kumfanya aseme neno litakalo mletea shida.Katika hali hii,Yesu alishinda, na mwana sheria akajaribu “kujidai,na kujitetea”akampa mtego mwingine, “Na jirani yangu ni nani”?

## ENDELEA NA LUKA MTAKATIFU 10:30-37.

> 30 Yesu akajibu akasema, mtu mmoja alishuka toka Yerusalemu kwenda Yeriko,
> akaangukia kati ya wanyang’anyi, wakamuvua nguo, wakamtia jeraha, wakaenda zao,
> wakimwacha karibu ya kufa. 31 Kwa nasibu kuhani mmoja alishuka kwa njia ile, na
> alipomwona alipita kando 32.Na mlawi vivyo hivyo, alipofika pale akamuona, akapita
> kando 33 lakini msamari mmoja katika kusafiri kwake alifika hapo alipo, na
> alipomwona alimhurumia, 34 akakaribia, akamufunga jeraha zake,akazitia mafuta na
> divai, akamupandisha juu ya mnyama wake, akamupeleka mpaka nyumba ya wageni,
> akamtunza. 35 Hata siku ya pili akatoa dinari mbili, akamupa mwenye nyumba ya
> wageni, akisema mtunze huyu, na chochote utakachogaramia zaidi, mimi nitakaporudi
> nitalipa 36. Waonaje wewe katika hao watatu, ni yupi aliyekuwa jirani yake yule
> aliyeangukia kati ya wanyang’anyi? 37 Akasema, ni huyo aliye mwonea huruma.
> Yesu akamwambia, Enenda zako, nawe ukafanye hivyo.

7. Wayahudi waliwachukia wasamaria. Je! Yesu alisema msamaria alifanya nini kilicho mfanya mshindi katika hadithi hii.

# Mwanamume mwenyewe

## MATHAYO MTAKATIFU 5:27-28

> Mmesikia kwamba imenenwa, usizini lakini mimi nawambia, kila mtu atazamaye mwanamke kwa kumutamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake.

8. Wanaume mara kwa mara hujisikia kulazimishwa kuonyesha ushujaa wao kama wanaume kwa kuwa na ushirika wa kimapenzi na wanawake wengi. Je! Jibu la Yesu kuhusu “tamaa katika moyo” inajibuje shida hiyo?

9. Je! Matukio haya yote yanauhusiano gani?



© Carrie A. Miles, 2012

## Umejifunza nini / changa moto za kitamaduni

10. Je! wanaume wana upungufu gani na wao huumiaje katika wazo kwamba ni lazima wapate nafasi ya juu na kutawala wenzao?

11. Wanaume: Ni misukumo ipi mikubwa unayohisi kuwa na tabia katika njia hizi? Utafanya nini kama suluhisho kwa hali hizi ambazo unajaribiwa au unasukumwa kuwa na taabia kwa njia hizi?

Wanawake: Umewahi tarajia mwanamume aliyekaribu na wewe kupata nguvu juu ya wenzake au kulipiza kisasi? Je tabia zako na matarajio yako yatabadilikaje kusaidia wanaume katika maisha yenu kupata uhuru wao katika kristo?

12. Kama wakristo, Jinsi gani na kwa nini tunawasamehe wanaotuudhi ?



© Carrie A. Miles, 2012

# SOMO LA 7 INAMAANISHA NINI KUWA BWANA?

Yesu alishutumu mapendekezo mengi ya wakati wake na wakati wa sasa kuhusu kinacho maanisha kuwa mwanamume. Mtu mpya katika kristo hahitaji starehe au pesa au kufanya mapenzi kiholela, au ajaribu kuwa juu ya watu wengine.

Kwa hivyo, inamaanisha nini kwa kumwita Yesu Bwana?

## "Wewe ndiwe Kristo-----"

**Marko Mtakatifu 8:27-33**

> Yesu---------akawauliza wanafunzi wake, akasema, watu hunisema mimi kuwa ni nani? 28 wakamjibu, Yohana mbatizaji, wengine, Eliya, mmojawapo wa manabii,29. Naye akawauliza, Na ninyi mnasema ya kuwa mimi ni nani? Petro akajibu, akamwambia, wewe ndiwe Kristo. 30 Akawaonya, wasimwambie mtu habari zake
>
> 31.Akaanza kufundisha kwamba imempasa Mwana wa Adamu kupatikana na mateso mengi, na kukataliwa, na wazee, na wakuu wa makuhani, na waandishi, na kuuwawa, na baada ya siku tatu kufufuka. 32.Naye alikuwa akinena neno hilo waziwazi. Petro akamchukua , akaanza kumkemea. 33. Akageuka, akawatazama wanafunzi wake, akamkemea Petro, Akasema, Nenda nyuma yangu, shetani, maana huyawazi yaliyo ya Mungu, bali ya wanadamu.

Wakati ya Yesu wayahudi waliamini kwamba Mungu angemleta masihi kurejesha Ufalme wa dunia kwa Israeli. Wayahudi walitarajia kiongozi kama Daudi au Sulemani, mfalme wa haki ambaye angewaweka huru kutokana na kuonewa na Warumi.

1. Wakati Yesu alitangaza ya kuwa yeye ndiye masihi, lakini kwamba atakataliwa na kuuawa, kwa nini Petro alimkemea?

Yesu alimjibu kamwambia "Nenda nyuma yangu Shetani"! Inatukumbusha jaribu la tatu katika Mathayo Mtakatifu 4:8-10 Ambayo inasema:- Kisha Ibilisi akamuchukua mpaka mlima mrefu mno, akamuonyesha miliki zote za ulimwengu, na fahari yake 9 akamwambia, haya yote nitakupa, ukianguka kunisujudia. 10. Ndipo Yesu alipomwambia, Nenda zako Shetani, kwa maana imeaandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako, Umwabudu yeye peke yake.

2. Kuna uhusiano gani kati ya Petro na makusudio yake kuhusu kile Masihi atakuwa na jaribu la tatu?



© Carrie A. Miles, 2012

## ENDELEA NA KUSOMA MARKO MTAKATIFU 8:34, 38

Akawaita mkutano pamoja na wanafunzi wake, akawambia,

Maana kila mtu atakayenionea haya mimi, na maneno yangu, katika kizazi hiki cha uzinzi na dhambi, Mwana wa Adamu atamuonea haya mtu huyo, atakapokuja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika watakatifu.

3. Kwa nini Yesu anasema wanafunzi wake watamwonea haya?

Kile ambacho Yesu alijaribu kuwafundisha wafuasi wake ni jinsi Mungu anavyotumia nguvu ni vigumu kwao kuelewa, ijapokuwa alirudia kila mara. Hata baada ya kusulubishwa kwake wanafunzi waliendelea na matarajio yao kuwa Yesu angekuwa mfalme wa ulimwengu. (Matendo ya mitume 1:6)

# Miguu Michafu

## YOHANA MTAKATIFU 13:3-10, 12-17

[Katika sikuku ya pasaka] yesu, hali akijua ya kuwa Baba amempa vyote mikononi mwake, na ya kuwa alitoka kwa Mungu naye anaenda kwa Mungu,4 aliondoka chakulani, kawaka kando mavazi yake, akatwaa kitambaa akajifunga kiunoni.5 .Kisha akatia maji katika bakuli, akaanza kuwatawadha wanafunzi miguu, na kuifuta kwa kile kitambaa alichojifunga.6. Hivyo yuaja kwa Simoni Petro huyo akamwambia, Bwana! wewe wanitawadha miguu mimi? 7. Yesu akajibu, akamwambia, nifanyalo wewe hujui sasa, lakini utalifahamu baadaye.8. Petro akamwambia, wewe hutanitawadha miguu kamwe. Yesu akamwambia, kama nisipokutawadha, huna shirika nami. 9. Simon Petro akamwambia, Bwana si miguu yangu tu, hata mikono yangu na kichwa changu pia. 10. Yesu akamwambia, yeye aliye kwisha kuoga hana haja ila ya kutawadha miguu, bali yu safi mwili wote, nanyi mmekuwa safi, lakini si nyote.

12.Basi alipokwisha kuwatawadha miguu, na kuyatwaa mavazi yake, na kuketi tena, akawambia, je!mmeelewa na hayo niliowatendea?13 Ninyi mwaniita, mwalimu na Bwana, nanyi mwanena vema, maana ndivyo nilivyo.14Basi ikiwa mimi, niliye Bwana na Mwalimu, nimewatawadha miguu, imewapasa vivyo kuwatawadha miguu ninyi kwa ninyi.15. Kwa kuwa nimewapa kielelezo, ili kama mimi nilivyo watendea, nanyi, mtende vivyo. 16. Amin, Amin, nawambia ninyi, mtumwa si



© Carrie A. Miles, 2012

> mkubwa kuliko Bwana wake, wala mtumwa si mkuu kuliko yeye aliyempeleka. 17.
>
> Mkijua hayo, heri ninyi mkiyatenda.

Kama ilivyo desturi za usafi wa baadhi ya wayahudi, kutawadha miguu kulikuwa ni hitaji la kawaida. Watu walikuwa wakivaa viatu vilivyo wazi, na miguu yao ilichafuliwa. Kwa maana watu walikula wakiketi kwenye majamvi yao, miguu michafu ingegunduliwa na kila mtu. Ilikuwa ni kitendo cha ukarimu kuwa na mtumwa mlangoni kuwatawadha miguu wageni. Kitendo cha kuwatadha miguu, hasa, kilichukuliwa cha chini sana ambacho hata mtumwa wa kabila ya Kiyahudi hakurusiwa kukifanya, kilifanyika na watumwa wa Kigeni au Kimataifa badala yake.

4. Kwa nini Petro alikasirika? Wakati yesu alichukua kazi ya mtumwa wa kiume au mtumwa wa kike, hii ilimaanisha nini kwa kile Petro angetakikana kufanya?

5. Kwa nini Petro anamuliza Yesu amtawadhe mwili wote?

Bartchy ana mawazo kwamba mume katika utamaduni wa aina hii anahitajika abadilishwe kabisa ili ajaribu tukio hilo liwe “kiroho”, ili kitendo hicho kiwe cha desturi badala ya kuwa kazi ya uchafu ambayo ingelihitajika kuitenda.

6. Onyesha wakati mwingine ambao Yesu alionyesha kwa neno au mfano, kwamba mawazo ya ulimwengu kuhusu mamlaka, heshima na nguvu haina sehemu katika ufalme wa Mungu.

7. Je! Unyenyekevu wa kikiristo ni ishara tu au ni jaribio? Je! Yesu alijinyenyekesha wakati wake wa maisha yake kwamba aweze kuwa na haki ya kuwa na “Bwana” milele au inatuhusu kila mmoja wetu?

> Wakristo wa kwanza walikiri, kwamba Yesu ni bwana, hukata kuwili. Kwanza, ukisema Yesu ni Bwana. Hii inamaanisha kwamba Sultani (au Rais au Askofu) hawezi kuwa Bwana, hii inamanisha kwamba baba yangu hawezi kuwa Bwana, hii inamanisha kwamba mume hawezi kuwa Bwana, Yesu ni Bwana. Sasa njia ya pekee ambayo ubwana unaweza kutafsiriwa vizuri---katika jamii ya kikiristo ni katika ile njia Yesu alichukua ubwana --------Yesu anajaza nafasi yote ya ubwana hamruhusu mtu mwingine hapo, na tena anateremka chini na anafanya kazi katika nafasi ya utumwa. Anatukaribisha sote tukutane naye hapo, wanaume na wanawake kama Bwana ni Yesu, nguvu zote si za kutawala wengine na vitu lakini ni kutia nguvu wasio na nguvu, kuwainua wote walioanguka, kupatanisha, kuumba nafasi za uponyaji, kutia moyo watu kukomaa na kuajibika na kurejesha jamii, Gundua: kinyume na utawala wa nguvu, aina hii ya nguvu hutolewa bila kikomo (Bartchy, 1999).

## Umejifunza nini / Changamoto za kitamaduni?

8. Yesu akijua kwamba Mungu amempa kila kitu mikononi mwake, alitumia mamlaka hayo kufanyia kazi ambayo wanafunzi wake waliona haina maana na akawauliza wajifunze kutoka kwa tabia yake. Hii inamaanisha nini kwetu jinsi inatupasa kutumia mamlaka yote juu ya wenzetu leo? Hii inamanisha nini kwa uhusiano kati ya mume na mke katika Kanisa na Familia?



© Carrie A. Miles, 2012

# SOMO LA 8 UHURU AMBAO KRISTO ANAWAPA WANAWAKE

Katika ulimwengu wa anguko, ni mambo gani ambayo wanaume wanataka au wanahitaji wanawake wao wawape au wawafanyie?

1)
2)
3)

Moja kati ya matokeo ya kuishi katika ulimwengu wa miiba na michongoma ni kwamba mwanamke anadhaminiwa sana kwa uwezo wake wa kuzaa na kutunza nyumba yake vizuri, naye anadhaminiwa kwa sababu ya ngono yake. Yesu sasa anatuachilia kutoka kwa matakwa yaliyotokea kwa sababu ya anguko. Anatuonyesha njia kutoka kwa matarajio ya uongo na kutuelekeza kwa kile kilicho cha mhimu kwa kila mmoja, mume au mke.

## Mke na kuzaa watoto

### LUKA MTAKATIFU 1:26-28, 30, 34, 35, 38

--------Malaika Gabrieli alitumwa na Mungu kwenda mpaka mji wa Galilaya, jina lake Nazarethi, kwa mwanamwali bikira aliye kuwa ameposwa na mtu, jina lake Yusufu,--------na jina lake bikira huyo ni Mariamu. Akaingia nyumbani kwake akasema---------------usiogope Mariamu, kwa kuwa umepata neema kwa mungu. Tazama, utachukua mimba na kuzaa mototo mwanamume, na jina lake utamwita Yesu. Mariamu akamwambia malaika, litakuwaje neno hili, maana simjui mume? Malaika akajibu akamwambia, "Roho Mtakatifu atakujia juu yako, na nguvu zake aliye juu zitakufunika kama kivuli" Mariamu akasema, "Tazama, mimi ni mjakazi wa Bwana, na iwe kwangu kama ulivyosema."

### KUMBUKUMBU LA TORATI 22:20-21

Lakini ikiwa ni kweli neno hili, la kutoonekana kwake yule kijana alama za ubikira, na wamtoe nje yule kijana mlangoni pa nyumba ya baba yake, na waume wa mji wake wampige kwa mawe hata afe.

1. Hatari gani ambayo Mariamu alikuwa anachukuwa kwa kukubali kumzaa mtoto ambaye hakuwa wa Yusufu? Mariamu kukubali hatari hii kunatuambia nini kuhusu tabia yake?

### LUKA 11:27-28

Wakati Yesu alisema haya, Mwanamke katika umati akapaza sauti yake na akamwambia,"limebarikiwa tumbo lililokuzaa na matiti uliyonyonya!" lakini akasema" wamebarikiwa wanaolisikia neon la Mungu na kulitii!"

2. Mwanamke alisema ni nini kilikuwa cha mhimu kwa mama wa Yesu?

3. Katika ulimwengu wa anguko, wanawake wanadhaminiwa kwa wingi wa vijana waliowazaa. Kwa kinyume, Yesu alisema kwamba ni nini cha muhimu kwa mama yake? Hii inamaanisha nini kwa kile Mungu anakichukua kuwa cha muhimu kwa mwanamke?



© Carrie A. Miles, 2012

## Mwanamke kama mfanyakazi

### LUKA MTAKATIFU 10:38-42

> Ikawa katika kuenenda kwao aliiningia katika kijiji kimoja, mwanamke mmoja jina lake Martha akamkaribisha nyumbani kwake. Naye alikuwa na umbu lake aitwaye Mariamu, aliyeketi miguuni pake Yesu, akasikiliza maneno yake, lakini Martha alikuwa akihangaika kwa utumishi mwingi, akamwendea, akasema, Bwana, huoni vibaya hivyo ndugu yangu alivyoniacha nitumike pekee yangu? Basi mwambie anisaidie. Bwana akajibu akamwambia, Martha, unasumbuka na kufadhaika kwa ajili ya vitu vingi, lakini kinatakiwa kitu kimoja tu, na Mariamu amelichagua fungu lililo jema, ambalo hataondolewa.

4. Maneno “kuketi miguuni” pa Mwalimu kulimaanisha kuwa mtu huyo anayeketi ni mwanafuzi. Wanawake hawakuwa wakifanya hivyo kwa kawaida. Je! Kukubali kwake Yesu kuhusu Mariamu katika tendo hilo, kunatuambia nini kuhusu nia yake kuelekea wanawake?

5. Yesu alilinganisha kufadhaika kwa Martha kama mkaribishaji wake na uchaguzi wa Mariamu wa kujifunza neno la Mungu. Je Yesu alimjibu nini bure Martha?

6. Je hadithi hizi mbili kuhusu akina Mariamu zina maneno yapi yanayofanana? Wanaume na wanawake wanaweza kujifunza nini kuzihusu?

## Umejifunza nini?

7. Hadithi hizi zinamaanisha nini kwa wanawake leo? Hadithi hizi zinamaanisha nini kwa wanawake waliokataliwa kwa sababu hawazai watoto au wanaozaa wasichana pekee?

8. Tutaepukaje “kufadhaika na kusumbuka” matarajio ya ulimwengu, kuhusu jinsi tutakavyokuwa kama wanaume au wanawake ili tujitoe kwa kile kilicho cha muhimu?

9. Wanaume, mtawekaje huru wanawake wenu kuketi miguuni pa Yesu?



© Carrie A. Miles, 2012

# SOMO LA 9 WANAWAKE WACHAFU

Katika ulimwengu wa mwanguko uhusiano wa ngono wa wanawake hufanyika mali ya wanaume.Tamaduni nyingi zimebuni sheria za kutunza haki za wanaume kwa uhusiano wa kingona wa wanawake,haswa nidhamu yake ambayo haimuruhusu mwanamke kuhusiana au kutembea kila siku na watu wengine. Mwishowe watu wengine wa hufikiria kumhusu mwanamke – na tamaa ya ngono ambayo hujisikia kwao – kama chanzo cha uovu wote. Wanawalaumu wanawake kwa tamaa ya wanaume, na wanaamini kuwa kumgusa mwanamke ni kitu kichafu. Hii ilikuwa kweli nyakati za Yesu. Mwanamume Myahudi angempa talaka mwanamke wake kwa kumuona anaongea na mwanamume mwingine njiani. Wanaume walishikwa katika utamaduni wa heshima / aibu, na tena waliwaona wanawake katika familia kuwa hatari katika heshima, kama mwanamke ambaye angefanya tabia mbaya angefikiriwa kuwa ameleta aibu kubwa katika familia. Yesu alishikilia viwango vya Biblia kuhusu matendo ya zinaa, lakini aliwashangaza watu wengi wakati mwingi alipokataa kuruhusu hofu ya wanawake kumzuia kuwahudumia – au kuwaweka kufanya kazi ya kueneza injili.

## « Kama angemjua ni nani anayemgusa »

### LUKA MTAKATIFU 7:36-39

Mtu mmoja katika mafarisayo alimwalika ale chakula kwake, nyumbani akaingia katika nyumba yake yule farisayo, akaketi chakulani. Na tazama, mwanamke mmoja wa mji ule, aliyekuwa mwenye dhambi, alipopata habari ya kuwa ameketi chakulani, katika nyumba ya yule farisayo, alileta chupa ya Marimari yenye marhamu. Akasimama nyuma karibu na miguu yake, akilia, akanza kumdondeshea miguu machozi yake, na kuipangusa kwa nywele za kichwa chake, akiibusu busu miguu yake na kuipaka yale marhamu.

Basi yule farisayo aliyemwalika alipoona vile, alisema moyoni mwake, mtu huyu kama angekuwa nabii, angemtambua mwanamke huyu amgusaye, ni nani, naye ni wa nanma gani, ya kwamba ni mwenye dhambi.

1. Kwa nini farisayo huyo alisumbuliwa?

### ENDELEA NA LUKA MTAKATIFU 7:40-47.

Yesu akajibu akamwambia, Simoni, nina neno nitakalo kukwambia. Akasema, mtu mmoja mkopeshaji alikuwa na wadeni wawili, mmoja amwia dinari mia tano,



© Carrie A. Miles, 2012

na wa pili hamsini. Nao walipokuwa hawana cha kumlipa, aliwasamehe wote wawili. Katika hao wawili ni yupi atakayempenda zaidi? Simoni akajibu akasema, nadhani ni yule ambaye alimsamehe nyingi. Akamwambia, umeamua haki akamgeukia yule mwanamke, akamwambia Simoni, wamwona mwanamke huyu? Niliingia nyumbani kwako, hukunipa maji kwa miguu yangu, bali huyu amenidondoshea machozi miguu yangu, na kuipangusa kwa nywele za kichwa chake. Wewe hukunibusu, lakini huyu tangu nilipoingia hakuacha kunibusu sana tangu miguu yangu, hukunipaka kichwa changu mafuta, bali huyu amenipaka miguu yangu marhamu. Kwa ajili ya hayo nakwambia, amesamehewa dhambi zake ambazo ni nyingi.

2. Yesu alifikiria nini kuhusu mwanamke aliyekuwa anamguza?

3. Je kulikuwako na jambo ambalo Yesu alifikiria kujizuia kutoka kwa wanawake?

## Mwanamke katika kisima

### YOHANA MTAKATIFU 4:7,9

Akaja mwanamke msamaria kuteka maji. Yesu akamwambia nipe maji ninywe. Basi yule mwanamke msamaria akamwambia, imekuwaje wewe Myahudi kutaka maji kwangu nami ni mwanamke Msamaria ?(Wayahudi hawashirikiani na Wasamaria).

Kulikuwa na chuki ya ndani kati ya Wasamaria na Wayahudi. Wayahudi walifikiria kuwa wanawake Wasamaria walikuwa wachafu na wananuka (Massy 1989) moja kati ya mambo muhimu ambayo mwanamke mchafu asingeruhusiwa kuguza ni vikombe vya maji ya kunywa – na Yesu alikuwa anauliza mwanamke huyu maji ya kunywa! Mwanamke huyu alishangazwa!

### ENDELEA NA YOHANA 4:16-18,25-26.

Yesu akamwambia, nenda kamwite mumeo, uje naye hapa. Yule mwanamke akajibu, akasema sina mume. Kwa maana umekuwa na wanaume watano, naye uliye naye sasa si mume wako, hapo umesema kweli. Yule mwanamke akamwambia najua ya kuwa yuaja masihi,--------naye atakapokuja, yeye atatufunulia mambo yote. Yesu akamwambia, mimi ninayesema nawe ndiye.



© Carrie A. Miles, 2012

4. Historia ya zinaa ya mwanamke huyu, ingemfanya mwanamume wa Kiyahudi amfukuze, jambo ambalo Yesu alijua. Hata alisema jambo lililo funua maneno yake. Je! kuelewa kwake Yesu kuhusu hali ya maisha yake kuliweza kudhuru moyo wa kutaka wa kuzungumza naye? Ni kitu gani anamfunulia huyu mwanamke?

## ENDELEA NA YOHANA MTAKATIFU 4:27

> Mara hiyo wakaja wanafunzi wake, wakastaajabu kwa sababu alikuwa akisema na mwanamuke-------

Katika utamaduni huu, wanaume na wanawake hawakuruhusiwa kuzungumza hadharani, hata katika siri hawakuwa na mengi ya kufanya pamoja. Wanaume wengine wangewapuuza wake zao na watoto wao wa kike hadharani ili mtu asiwasikie kuwa wanafanya tabia mbaya. Wanafunzi walishangazwa.

Mwanamke Msamaria alirudi katika kijiji chake na akawa wa kwanza kushuhudia Kristo. Yohana Mtakatifu 4:39-42 inatuambia kuwa matokeo ya mazungumzo ya Yesu na mwanamke kwenye birika, yalisababisha watu wengi kumujua Bwana.

# Viwango viwili

## YOHANA MTAKATIFU 8:3-11

> Waandishi na mafarisayo wakamletea mwanamke aliyefumaniwa katika uzinzi, wakamweka katikati. Wakamwambia, Mwalimu, mwanamke huyu amefumaniwa alipokuwa akizini. Basi katika torati Musa alituamuru kuwapiga kwa mawe wanawake wa namna hii, nawe wasemaje?
>
> Nao wakasema neno hilo wakimjaribu, ili wapate sababu ya kumshitaki lakini Yesu akainama, akaandika kwa kidole chake katika nchi. Nao walipozidi kumhoji alijiinua, akawambia, yeye asiye na dhambi miongoni mwenu na awe wa kwanza kumtupia jiwe. Akainama tena, akaandika kwa kidole cha incha yake. Nao waliposikia wakashitakiwa na dhamiri zao, wakatoka mmoja kwa mmoja, wakianzia tangu wazee hata wa mwisho wao, akabaki Yesu peke yake na yule mwanamke amesimama katikati, Yesu akajiinua asimwone mtu ila yule mwanamke, akamwambia, mwanamke, wako wapi wale washitaki wako? Je! Hakuna aliyekuhukumu kuwa na hatia? Akamwambia, hakuna, Bwana. Yesu akamwambia, wala mimi sikuhukumu. Enenda zako, wala usitende dhambi tena.

5. Unafikiri kwamba Yesu alikuwa anaandika nini katika nchi?



© Carrie A. Miles, 2012

Msomi wa Agano jipya S. Scott Bartchy anachangia na kusema, “yuko wapi huyo mwanamume” kwa kuwa uzinzi hufanyika na watu wawili.

6. Yesu akawambia wanaume, “yeye asiye na dhambi miongoni mwenu na awe wa kwanza wa kumtupia jiwe”. Je! Mwitikio huu unaleta changa moto gani katika utamaduni wa viwango viwili hivi? (utamaduni wa viwango viwili ni utamaduni wa kuamini kuwa zinaa ni kosa la wanawake, lakini ni sawa kwa wanaume hata wakifanya zinaa.)

# “Tamaa ya Moyoni”

## MATHAYO MTAKATIFU 5:27-28

> Mmesikia kwamba imenenwa, usizini, lakini mimi nawambia, kila mtu atazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake.

7. Yesu anawasihi wanaume wakome kufanya nini? Ni nini ambacho Yesu anakilaumu kwa tamaa ya mwanamume, mwanamke au mwanamume?

8. Maisha ya wanawake ingekuwaje tofauti kama wanaume wangetii Yesu na kuacha kuwatamani wanawake?

Katika kila matukio haya, Yesu akakumbushwa hofu ambayo ingezuia huduma yake kwa wanawake na kuwazuia wanawake kuja katika uhuru na nafasi katika ufalme wa mbinguni. Alipuuza kwa nguvu hofu hiyo. Hata anawambia wanaume kuwachukuwa wanawake kama vyombo vya kutosheleza mahitaji ya wanaume ilikuwa dhambi kubwa yenyewe.

# Kwa ujumula

Katika ulimwengu wa mwanguko, wanawake wanadhaminiwa kwa sababu ya miili yao na uwezo wao wa kuzaa watoto, wafanye kazi, na kutosheleza mahitaji ya wanaume(ngono). Yesu alifundisha kuwa thamana ya wanawake ilikuwa ni zaidi kuliko vitu hivi vyote. Alisema kuwa dhamana ya kweli ya mwanamke huwa katika ushirika wake na Mungu. Kama anavyofanya na wanaume, Yesu anatuambia kuwa mke mpya katika Kristo yuko huru kutafuta kwanza ufalme wa Mungu.

# Umejifunza nini

9. Je! Kazi yako itakuwaje nzuri shuleni, kanisani au katika familia wanaume na wanawake wangefanya pamoja bila kufikiria kuhusu ngono.



© Carrie A. Miles, 2012

# SOMO LA 10 PAULO NA MAMLAKA NYUMBANI

Katika barua ya Waefeso, mtume Paulo anafafanua mafundisho ya Yesu jinsi ya kuishi umekombolewa kutoka ulimwengu wa anguko. Ijapokuwa Paulo analaumiwa kwa kupendelea utawala, ni kutoelewa maandiko yake. Tunapoangalia kwa karibu, waefeso 5,6, tunaona kwamba badala ya kupendelea utawala, Paulo anamfuata Yesu kwa kukataa kabisa.

Utamaduni huweka mzigo kwa wanaume kwa kuwambia kwamba, "mwanamume kamili au mwenyewe" anatakiwa awe na uongozi na mamlaka juu ya watu wengine. Hata mwanamume akiwa maskini na hawezi kuwaongoza wanaume wengine, utamaduni unasema kuwa ni lazima awe na mamlaka katika nyumba yake mwenyewe.

Lakini Yesu alifundisha kuwa wakristo hawaruhusiwi kuongoza kwa nguvu na kuwa na mamlaka juu ya watu wengine. Katika somo hili, tutaona vile mtume Paulo anavyotumia mafundisho ya Yesu kinyume cha kutumia mamlaka ya kidunia badala yake kuwa na uhusiano wa kijamii. Tunaanza na mamlaka yenyewe – yanayohusu uhusiano: utumwa.

## Paulo na Utumwa

Paulo aliwandikia barua watu walioishi katika miji ya utawala wa Kirumi wakati wake, Warumi walitawala Ulaya yote, Bahari ya Shamu na Kaskazini ya kati. Jumuia ya Kirumi iliundwa kwa kikundi kidogo cha watu wenye nguvu waliongoza vikundi vikubwa vya watu wengine – wanawake wao, watoto na watumwa. Neno kamili la familia katika Roma lilijumuisha watumwa wa mtu, watumwa wanaoishi katika sehemu moja na bwana mkubwa, mke wake, na watoto wake. Zaidi ya theluthi kufika nusu ya watu wa Ugiriki, Italia na katika mji kama Korintho walikuwa watumwa, na theluthi nyingine walikuwa wakati mmoja watumwa. Kuelewa kile Paulo anasema, kuhusu unyenyekevu katika familia tutaangalia kwanza vile anavyosema kuhusu jinsi ya kuwachukua watumwa. Tena tutasoma kile Paulo anawambia watoto, wanawake, na hatimaye mafundisho yake ya ajabu kwa mabwana, wazazi, na wanaume.

## Mausia kwa watumwa

### WAEFESO 6:5-8

> Enyi watumwa, watiini wao walio bwana zenu kwa jinsi ya mwili, kwa hofu na kutetemeka, kwa unyofu wa moyo, kana kwamba ni kumtii Kristo, wala si kama watumwa wa macho tu kama wajipendekezao kwa wanadamu bali kama watumwa wa Kristo mkitenda yampendezayo Mungu kwa moyo, kwa nia njema kwa kumtumikia Bwana wala si mwanadamu, mkijua ya kuwa kila neno jema alitendalo mtu atapewa lilo hilo na Bwana kwamba ni mtumwa au kwamba ni huru.

1. Je! Paulo anawambia watumwa watendeje katika waefeso 6:5-8? Orodhesha maneno ambayo watumwa wanatakiwa wafanye katika mchoro wa sanduku hapo chini. (Utajaza katika vijisanduku vingine baadaye). Inawabidi watumwa wawatii akina nani? Anatakiwa afanye matendo ya "hofu na kutetemeka" na "unyofu wa moyo kama kumfanyia nani"?



© Carrie A. Miles, 2012

| | | |
|---|---|---|
| Watumwa | Watoto | Wake |
| Akina bwana | Akina baba | Wanaume |

## Mausia kwa watoto

### WAEFESO 6:1-3

> Enyi watoto watiini wazazi wenu katika Bwana, kwa maana hii ndiyo haki, waheshimu baba yako na mama yako, amri hii ndiyo amri ya kwanza kwenye ahadi, upate heri, ukae siku nyingi katika dunia.

2. Paulo anawauliza watoto wafanye nini? Tena orodhesha maneno ambayo watoto wanatakiwa wafanye katika kijisanduku mahali wameandika "watoto" hapo juu. Kwa nini watoto inawabidi kufanya hivi?

## Mausia kwa wake

### WAEFESO 5:21-24,33

> Hali mnanyenyekeana katika kichwa cha Kristo. Enyi wake, watiini waume zenu kama kumtii Bwana wetu. Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha Kanisa, naye ni mwokozi wa mwili. Lakini kama vile Kanisa limtiivyo Kristo vivyo hivyo wake nao wawatii waume zao katika kila jambo.
>
> -----------mmoja kwa mmoja, kila mtu-------------mke asikose kusitahi mumewe.

3. Paulo anawauliza wanawake wafanye nini? Jaza katika kijisanduku maneno ambayo wake wanatakiwa wafanye mahali wameandika wake kwa kijisanduku hapo juu.

4. Kuna utofauti gani kati ya kile wanaambiwa wake kufanya na kile watoto na watumwa wafanye ?

Ijapokuwa tafsiri nyingi za Bibilia huweka nafasi katika kifungu cha 21 na cha 22 lakini vifungu hivi viwili ni sehemu ya sentensi moja. Kifungu cha 22, hakika hakina kitendo katika tafsiri ya kwanza, lakini ni sehemu ya kifungu cha 21. Paulo hawaulizi wanawake wanyenyekee pekee yao lakini wakristo wote wanaume na wanawake wanaulizwa "wanyenyekeane mmoja kwa mwingine" gundua kwamba wanawake wanaulizwa



© Carrie A. Miles, 2012

kunyenyekea badala ya kutii. Katika kiingereza na lugha yako ya nyumbani kunaweza kuwa na utofauti kidogo kati ya kunyenyekea na kutii.

Hata hivyo tutaona katika somo la 11 kwamba katika Kiyahudi, lugha ambayo Paulo aliandika, neno linalotafrisiwa ni "kunyenyekea" haikumaanisha kutii au kukubaliana na mtu mwingine lakini Paulo alikuwa akiwauliza wakristo wamfuate Yesu kwa kufanya uchaguzi wa lengo wa kuondoka kutoka kunga'ng'ana kwa kidunia kupata nguvu juu ya kila mmoja.

5. Je! Wake kwa nini wafanye hivi?

Watumwa, watoto na wake hawakuwa na haki au walikuwa na haki ndogo. Utiifu wao kwa mabwana zao, wazazi au wanaume wao, ulihitajika kwa Sheria ya Kirumi: hata mwanamume wa Kirumi angekuwa mtumwa au mtoto asiyetii. Watumwa wengi, wake na watoto waliokomaa walifanya yote wangefanya kulinda au kupata faida yao wenyewe, kwa njia ya ujanja au udanganyifu [Watumwa wa macho kuwapendeza watu.] Paulo anawaambia wakristo kwamba wasitende vitendo vyao kwa hofu, kulazimishwa au kujinufaisha wao tena. Bali wangetakiwa kufanya kazi zao kwa njia kwamba wanamtumikia Mungu na kuonyesha heshima kwa Kristo.

# Mausia kwa akina bwana

## WAEFESO 6:9

> Nanyi akina bwana, watendeeni wao yayo hayo, mkiacha kuwaogofya, huku mkijua ya kuwa yeye aliye Bwana wao na wenu yuko mbinguni, wala kwake hakuna upendeleo.

6. Paulo anawambia akina bwana "Wawatendee wao yayo hayo"Watumwa wao yale wanayo taka watumwa wao wawatendee akina bwana. Maneno haya yalikuwa ni yapi? Ni mambo yapi mengine ambayo anawaambia akina bwana kufanya?Andika maneno hayo katika kijisanduku chini ya Akina bwana hapo juu.

7. Inamaanisha nini "wala kwake [bwana] hakuna upend Leo?

# Mausia kwa akina baba

## WAEFESO 6:4.

> Nanyi akina baba, msiwachokoze watoto wenu, bali waleeni katika adhabu na maonyo ya Bwana.

8. Katika waefeso 6:1-3, Paulo anawambia watoto wawaheshimu na kuwatii baba yao na mama yao. Anaendelea kuwambia akina baba pekee yao katika kifungu cha nne katika ulimwengu wa anguko, kazi ya wana ni kuleta utukufu na heshima kwa kizazi chao. Katika Rumi, utiifu wake kwa wazazi kulihitajika kama Sheria, na mtoto asiyetii angeuawa. Kwa kinyume na hayo, kifungu hiki kinatuambia nini kuhusu makusudi ambayo akina baba wakristo wanatumia utiifu na heshima ya watoto wao? Yaandike maneno ambayo akina baba wanahitajika kufanyia watoto wao kwenye kisanduku hapo juu.



© Carrie A. Miles, 2012

## Mausia kwa Wanaume

### WAEFESO 5:25-33

{agape katika Kiyunani, kumaanisha kuwa na kutunza kitu}
Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda kanisa, akajitoa kwa ajili yake, ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno, apate kujiletea Kanisa utukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lolote kama hayo, bali liwe takatifu lisilo na mawaa. Vivyo hivyo imewapasa waume nao kuwapenda wake zao kama miili yao wenyewe. Apendaye mkewe hujipenda mwenyewe. Maana hakuna mtu anaye chukia mwili wake po pote bali huulisha na kutunza kama Kristo naye anavyolitendea Kanisa. Kwa kuwa tu viungo vya mwili wake kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake, na ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili mmoja. Siri hiyo ni kubwa, ila mimi nanena habari ya Kristo na Kanisa lakini kila mtu ampende mkewe kama nafsi yake mwenyewe--------------

Wanaume wa Kirumi, walikuwa na haki, jukumu ya kuwatiisha, kuwaogofya , na kuwatawala watumwa wao, na wake zao. Ndoa ilitengenezwa na akina baba kuendeleza matakwa yao wenyewe, bila kuwa na haja ya kujua vile bwana harusi na bibi harusi wanajisikia. Asilimia hamsini ya bibi harusi walikuwa ni wasichana wa miaka 12 wakiolewa na mume wa miaka 20 au zaidi ya miaka 30 au zaidi.

Wasikilizaji wa Paulo walikuwa na ujuzi mdogo kuhusu mapenzi au ndoa iliyojaa mapenzi. Wanawake wa Kirumi walitarajiwa kuwapa bwana zao warithi (hasa vijana kawaida) na kutunza nyumba zao. Wanaume katika utamaduni wa heshima / aibu walitoa nguvu zao kwa kupokea nafasi ya juu kwa ajili ya familia zao huku wakiwanyanyasa wengine. Mwanamke aliyetoka kwa familia nyingine, huchukiwa kwa kushushwa. Hakika, wake walihitajika kupeana heshima yao ya kwanza kwa baba zao zaidi ya wanaume wao. Mwanamke angetumainiwa wakati angemzaa mwana wa kiume. Ndoa haikuwa inatarajiwa kuwa ya kujisikia na kuwa ya ukaribu mke na mume kama Mrumi angekuwa na shida, mume au mke angetafuta ushauri kutoka kwa ndugu yake lakini sio yule wanaye kaa naye (mchumba).

9. Paulo anawambia wanaume wawachukuaje wanawake wao? Andika maneno hayo katika kijisanduku hapo juu chini ya akina baba.

10. Angalia maneno uliyoyandika ya watumwa na akina bwana, wake na wanaume na watoto wa akina baba. Kwa kuona kwako, je Paulo alitetea utawala wa nguvu au aliuliza mambo mengine tofauti?

Mambo ambayo Paulo aliwaambia wanaume wakristo kufanya –kuwatunza watoto wao na wake wao! Wajitoe wao kwa watu wengine! Waache kutumia nguvu za ulimwengu kwa watumwa kinyume na jinsi utamaduni wao ulivyo wahitaji wanaume kufanya.



© Carrie A. Miles, 2012

Ushauri wa Paulo kwa watumwa, watoto na wake wagundue mamlaka, ya ulimwengu kwa bwana wakubwa haingewezekana kukataliwa au kuepuka watu hawa wote walifungwa na Sheria za Kirumi.

Badala ya kuambiwa wanaume wakristo kuwa na jukumu ya kuwatala familia zao, au kwamba wana haki ya kuwatumia kwa matakwa yao wenyewe, Paulo aliwambia jinsi wakristo wanaweza kutumia mamlaka mbayo mila zao zimewapa. Alisema, kama unataka uwe bwana mkubwa au bwana, inakubidi uwe bwana kama Yesu alivyokuwa.

> {Baada ya Yesu kuja}------------njia ya pekee ambayo ubwana unatafsiriwa vizuri---------katika jamii ya kikristo ni kwa njia Yesu alivyo uchukua ubwana--------Yesu alijaza nafasi yote ya ubwana wake, hakumruhusu mtu yeyote katika nafasi yake, baadaye yeye anakuja na kufanya kazi katika nafasi ya mtumwa.Anawakaribisha watu wote tukutane naye hapo, wanaume na wanawake [Bartchy 1997]

Kujitolea kwenyewe kwa mkristo ni kuachilia nafasi na cheo alichopewa kama jamii inakufanya uwe bwana, mkristo(wa aina ya Paulo) inabidi mwitikio wake ni kuwa mtumwa badala yake.

| **Watumwa** | **Watoto** | **Wake** |
|---|---|---|
| Utumike kwa uaminifu (si kwa utumwa wa macho tu)<br><br>wamtumikie<br><br>Mungu kwa nguvu zao zote ijapokuwa ni watumwa. | Wawatii wazazi wote. | Wajinyenyekeshe wawachukue wanaume wao kwa heshima. |
| **Akina bwana**<br><br>Wafanye kama vile watumwa wanavyo wafanyia wasiwaogofye (wasitumie nguvu za kimabavu)<br><br>Kumbuka Mungu hatambui akina bwana, wakuu wa ulimwengu. | **Akina baba**<br><br>Usiwachokoze watoto(usitumie nguvu za kimabavu)<br><br>Watunze na kuwalea katika njia ya Bwana. | **Wanaume**<br><br>Upendo wa ***Agape*** wawapende kama miili yao / wajitoe wao kwa wake zao wawafanye watukuzwe wawatunze na kuwalinda waache baba zao na mama zao wawe na wake zao. |

## Umejifunza nini?

11. Kwa nini unafikiri kwamba Paulo alihisi kuwatia moyo wanawake wa wanaume wanaomfuata Kristo wawastahi ( kifungu cha 33).

12. Mausia ya Paulo yanamaanisha nini jinsi wazazi wanatakikana kuwachukua watoto wao? Jinsi gani watu wanatakikana kuwachukua watumishi nyumbani mwao? Jinsi gani waliooana wanatakikana kuchukuliana mmoja kwa mwingine?



© Carrie A. Miles, 2012

# SOMO LA 11  MTUME PAULO NA "UBWANA "

Mafundisho ya Paulo kuhusu ndoa yalikusudia kuwarudisha mume na mke katika uhusiano wa kweli wa kuumbwa kwao. Ili kuelewa jinsi mafundisho ya Paulo yanatuweka huru, inatubidi tushinde vizuizi vya mila vilivyoletwa kwa sababu ya anguko.Kuelewa vizuri matumizi ya neno hili "kichwa" kuelewa uhusiano wa mume kwa mke wake ni hatua ya kwanza ya muhimu.

## "Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe…"

## WAEFESO 5:20-23

> …….kumshukuru Mungu Baba siku zote kwa mambo yote, katika jina lake Bwana wetu Yesu Kristo, hali mnanyenyekeana katika kicho cha Kristo.Enyi wake watiini waume zenu kama kumtii Bwana wetu.Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha Kanisa, naye ni mwokozi wa mwili.

1. Watu huelewa nini kuhusu neno hili "Kichwa" katika kifungu hiki?

2. Kifungu hiki kinaweza kuelewekaje katika utamaduni kuonyesha uhusiano uliopo kati ya mume na mke?

Katika lugha nyingine, neno "Kichwa" lina maana hii "kiongozi", "bwana mkubwa", au "aliye na nguvu zote".Neno ambalo Paulo alitumia halikuwa mojawapo ya maneno hayo.

Neno lililotumiwa hapa ni ***Kephale*** (***kef-ah-LAY***) linamaanisha kwa kawaida kitu kilicho juu ya kingine, kama kichwa cha maandiko kwenye karatasi. Maana yake ya kawaida ni jinsi ilivyo mwili, kichwa cha mtu kweli angemaanisha "chanzo", kama chanzo cha moto. Ilikuwa pia ni lugha ya jeshi, kwa kuwa mwana jeshi aliyetangulia wenzake – sio amiri jeshi, bali yule aliye katika nafasi ya hatari zaidi. Wakati Paulo aliandika, *kephale* haikumaanisha mamlaka juu ya, kiongozi, bwana mkubwa, mwenye kiti au mtawala.

Hata katika Agano jipya wakati waandishi walimaanisha kiongozi au mtawala, walitumia neno lingine, ***archon***. Kama mwandishi alimaanisha "mamlaka" kwa kawaida, angetumia neno Exousia. Maneno mengine Paulo angeweza kutumia [lakini hakuyatumia] inajumuisha maneno kama kyrios [bwana] au despotis [pia hutafsiriwa "bwana" au kichwa cha nyumba."]

Hakuna kati ya maneno haya Paulo aliyatumia kuonyesha uhusiano kati ya mke na mume katika wefeso 5 au  1 Wakorintho 11. Tunapoendelea kujifunza tutaona kwamba mwanamume kuwa kichwa cha mke wake ni kitu cha ajabu lakini Paulo hakusudii matumizi ya neno kichwa kumaanisha mume anatakiwa kuonyesha mamlaka yoyote juu ya mkewe.



© Carrie A. Miles, 2012

## “---kama Kristo alivyo Kichwa cha Kanisa-----”.

Mwanamume amesemwa kuwa kichwa cha mkewe mara mbili katika agano jipya, lakini Yesu amenenwa kuwa kichwa cha kanisa mara mingi. Tukielewa kile kinachomaanisha Yesu kuwa kichwa cha Kanisa itazidisha kuelewa kwetu Paulo anavyosema kichwa / mwili katika ndoa.

Waefeso 1:9-10 inatumia neno lililorudiwa kueleza kile Paulo alimaanisha.

### WAEFESO 1:9-10

Akisha [Mungu] kutujulisha siri ya mapenzi yake, sawasawa na uradhi wake, alioukusudia katika yeye huyo. Yani kuleta madaraka ya wakati mkamilifu,[kuunganisha] au kuleta pamoja] atavijumulisha vitu vyote katika Kristo, vitu vya mbinguni, na vitu vya dunia pia. Naam, katika yeye huyo. [maneno mengine yameongezewa kusisitiza.]

Neno lililotafsiriwa “kuunganisha” ***anakephalaio***, “kuanza” neno linatafsiriwa kama “kumaliza” “kuunganisha” au “kuvileta vitu tofauti pamoja katika umoja.” [ona ***kephale*** katika *ana**kephal**aio?]*

Ukikumbuka katika mawazo yako maana ya “kichwa” kama mtu anaye “leta vitu pamoja katika umoja” gundua vifungu vifuatavyo kumuhusu Kristo kama kichwa.

Wakolosai 1:17-18: Naye amekuwako kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikana katika yeye, naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha Kanisa----”

Wakolosai 2:19: [Paulo anaongoea kuhusu mtu anayefuata “maneno yasiyo na maana”] wala hakishiki kichwa ambacho kwa yeye mwili wote ukiruzikiwa??? na kuungamanishwa kwa viungo na mishipa, hukua kwa maongeo yatokayo kwa Mungu.

Waefeso 4:15: [Paulo anatuambia sisi katika Kristo si watoto wachanga wa kutupwa huku na huku] “lakini hushika kweli katika upendo na kukuwa hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo. Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja hukuuza upate kujijenga wenyewe katika upendo.

Wakolosai 2:9-10: “maana katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili na ninyi mmetimilika katika yeye aliye kichwa [***kephale***] cha enzi yote [***arche***] na mamlaka.”



© Carrie A. Miles, 2012

Wefeso 1:22: “akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa, juu ya vitu vyote kwa ajili ya Kanisa ambalo ndilo mwili wake ukamilifu anaye kamilika kwa vyote katika vyote.

3. Inamaanisha nini “kichwa” katika vifungu hivi?

Waefeso 1:22 ni ya mhimu kwetu tukijaribu kuelewa utofauti uliopo kati ya “kichwa” kama mtawala na kichwa kama mtu anayeunganisha au kuvifanya vikue. Katika kifungu hiki Kristo ni mmoja na Kanisa, ambalo ndilo mwili wake na utimilifu wake. Vitu vilivyo wekwa chini ya Kristo viko chini ya miguu yake sio kichwa chake. Hio kuumaanisha kuwa kichwa hakiwezi kuweka chini, kutawala au kuongoza mwili lakini anatawala pamoja katika umoja wa mwili.

Msomi wa Kiyunani Richard Cervin aliandika “kwa hivyo Paulo anamaanisha nini akitumia neno kichwa katika barua zake? Hamaanishi, “mamlaka juu ya” Kama chombo cha kitamaduni, au hamaanishi, ‘chanzo’ kama chombo cha waandishi, ninafikiria kuwa anatumia hali ya maumbile yani kichwa cha mwili.

Kichwa + Mwili = Mwili Mmoja.

## WAEFESO 5:20-31

Gundua vile Paulo anatumia maneno haya Kichwa/Mwili katika vifungu hivi.

20 na kumushukuru Mungu baba siku zote kwa mambo yote katika jina lake Bwana wetu Yesu Kristo, 21 hali mnanyenyekeana katika kicho cha Kristo. 22 Enyi wake watiini waume zenu kama kumutii Bwana wetu, 23 kwa maana mume ni kichwa cha mkewe naye ni kichwa cha Kanisa, naye ni mwokozi wa mwili, 24 lakini kama vile Kanisa limtiivyo Kristo, vivyo hivyo wake nao wawatii waume zao katika kila jambo.

25 enyi waume, wapendeni wake zenu kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake, 26 ili makusudi aitakase kwa ajili yake, 27 apate kujiletea Kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyazi wala lolote kama hayo, bali liwe takatifu lisilo na mawaa 28 vivyo hivyo imewapasa waume nao kuwapenda wake zao kama miili yao wenyewe, 29 maana hakuna mtu anayeuchukia mwili wake po pote 30 kwa kuwa tu viungo vya mwili wake 31 kwa sababu hiyo mtu atamwacha mama yake na baba yake, ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili mmoja.



© Carrie A. Miles, 2012

4. Itatusaidiaje kuelewa mausia ya paulo kwa wanaume katika Waefeso 5:25-31 alipotumia neno kephale {kichwa} kilicho kama “muumbaji wa umoja” [watu wawili kuja katika umoja] badala ya “mamlaka juu ya”?

5. Katika vifungu hivi, ni nini ambacho mume anasitahili kufanya ambacho kinafanana na Yesu kama kichwa cha Kanisa [hapo katika vifungu ambavyo tumeviandika hapo awali katika somo hili?]

6. Ni nini kitatokea katika uhusiano wakati mwanamume anatafuta umoja na kukuza ndoa?

Kuwa “kichwa” sio kutunukiwa bali ni kujitolea, inambidi mwanamume aweke matakwa ya mkewe kwa kiwango kimoja na chake. Paulo anawaambia wanaume kumfuata Yesu, aliye mfano wao kama kichwa “alijitoa mwenyewe kwa Kanisa” inafanana na “mwokozi” [kifungu cha 23] alikuwa mtu aliyejitoa faida kubwa kwa mwingine, wakati mwingine kwa gharama kubwa yake mwenyewe.

Shida nyingine ambayo wakati mwingine tunayopata katika kuelewa kile Paulo alikuwa akisema katika mafundisho yake kwamba wan awake lazima “wawatii” waume zao.Fikiria kwamba mwanamume kuacha haki zake za ulimwengu za kumtawala mkewe, na kuacha kuongoza na kutawala bali awe katika umoja pamoja naye.Je!wakati mwingine hutendeka kwamba mwanamke anaweza kuogopa wakati mwanamume anaanza kutenda kama mkristo?kwamba anaweza kumdharau au kumchezea?

## Lakini kwa nini “mume asiwe mguu” ?

Kama Paulo anamaanisha kuwa mume na mke wote ni sawa na wako katika kiwango kimoja na wameungana, swali ni kwa nini mume ameamuwa kuwa kichwa, badala ya mwili, mguu au moyo. Cervin anasema Paulo alitumia “kichwa”kutuelezea kuwa kichwa ndicho chaenda mbele kwanza. Kulingana naye, mwanamume ndiye anatakiwa kuwa wa kwanza katika watumishi.

Tutachukua maelezo haya baadaye zaidi. Utumishi ulikuwa ni kwa wanawake. Kujitolea kwa mwanamke hakukuonyesha kuwa yeye ni mkristo, kwa kuwa ilikuwa ni jukumu lake la maisha. Kwa akili utiifu ulihitajika kama Sheria. Kwa hivyo wachumba kufanya uhusiano wao kwa umoja, ilimlazimu mwanamume kuwa kichwa-wa kwanza kuachilia nafasi-kwa sababu mwanamke hakuwa na mamlaka ya kuachilia. Kwa mwanamume kazi kama hii ilikuwa kujitolea kwa vile alikuzwa akitarajia hivyo. Hii ni kinyume na mafundisho ya Paulo kwamba Yesu kama kichwa cha kanisa “alijitoa kwa ajili yake”Wakati mwanamume anafanya hivi, paulo anatueleza kuwa haya yote yanatoka kwa upendo wa kikristo.

> “Kwa sababu mwanamume anaendelea kumpenda mkewe kwa kujitolea kama mwili wake katika ndoa, kwa marudio mwanamke mkristo anajitolea kwa dhati kwa mumewe katika uhusiano huo huo wa unyenyekevu wa utumishi unaoonyesha umoja wao. Kutokuweka mamlaka haya katika nafasi yake kunaweza kufanya ndoa kuwa kama ya watu wasioami na Kristo/Kanisa lake kuwa kama wasioamini isio ya muhimu….unyenyekevu ndio mwitikio halisi wa utumishi.Hi ndio maana halisi ya utiifu uliokomaa. (Gilbert Belezikiah, 1985, uk 159,161)



© Carrie A. Miles, 2012

## Umejifunza nini?

7.  Je! Kuelewa huku kuhusu kile Paulo anasema kuhusu ugumu katika ndoa ya kikristo inatujengaje au inatuchanga moto vipi katika uhusiano wetu sisi wenyewe?

8.  Wanaume, mtafananaje na Yesu katika kuumba umoja na mkeo?

Wake, mtaonyeshaje heshima kuu na usaidizi kwa mume wako anavyo mfwata Kristo?



© Carrie A. Miles, 2012

# SOMO LA 12 UNYENYEKEVU

Sehemu moja ya maandiko ya Paulo iliyo ya muhimu katika kuelewa nia ya mkristo kuhusu mamlaka huwa katika kuelewa kile alicho maanisha aliposema wanawake wawatii waume zao.

## Nyenyekeeni

### WAEFESO 5:21-22 NA WAKOLOSAI 3:18

Hali mmenyenyekeana katika kicho cha Kristo. Enyi wake watiini waume zenu kama kumtii Bwana wetu.

Wives, submit yourselves to your husbands, as is fitting in the Lord.

1. Je! Kifungu hiki kinaelewaje?

Sehemu moja ya matatizo tuliyonayo katika kuelewa Paulo ni katika neno “unyenyekevu” au “kujinyenyekeza” ilikuwa na maana mbaya katika Kiingereza. Katika Kiingereza mtu mnyenyekevu hufikiriwa kuwa mtu duni, mdhaifu, mpole, asiye na neno, asiye na nguvu au mamlaka, au aliye kama mtoto, au aliye kufa moyo katika maisha. Katika lugha nyingine nyingi, kujinyenyekeza ni kuwa mtu wa chini na mara kwa mara mtu huyo hutarajiwa kutii bila swali.

2. Katika lugha yako; neno unyenyekevu lina maana gani?

Njia tunayotumia kutafsiri neno “unyenyekevu”, au “kujinyenyekesha kwa” katika Kiingereza siyo sawa vile Paulo alivyo litumia. Barua za Agano Jipya, zina washauri watu wote “kunyenyekeana”. Wakristo kwa viongozi wao [Wahebrania 13:17] na katika mamlaka ya Kitaifa [Waraka wa kwanza wa Petero 2:13, Tito 3:1, Warumi 13:1], vijana kwa wazee [ Waraka wa kwanza wa Petero 2:18], kwa Mungu [Yakobo 4:7] na kwa Kanisa kwa Kristo [Waefeso 5:24]

Katika sehemu hizi zote neno “jinyenyekeze” halina maana ya “utiifu”, kukata tamaa, kuacha makusudi yako na kufuata ya mwenzako au kufanyia katika nafasi ya udhaifu [Walters, 1997, kittle, 1964]

## Mnyenyekeane

“Wake watiini waume zenu” husemwa mara nyingi kama ni mtu mmoja ndiye anayestahili kutii ukweli wa mambo ni kuwa kifungu cha Waefeso 5:22 sio kifungu kamili, au wazo kamili. Ijapokuwa tafsiri nyingi za kisasa hugawanyisha kifungu cha 21 na kifungu cha 22, lakini vifungu hivi viwili katika tafsiri ya kwanza ni sentensi moja. Katika tafsiri ya kiyunani,nusu ya sentensi amboyo ni ya kifungu cha 22 haina neno kutii kabisa :



© Carrie A. Miles, 2012

> 20 na kumshukuru Mungu Baba siku zote kwa mambo yote, katika jina la Bwana wetu Yesu Kristo, 21 hali mnanyenyekeana katika kicho cha Kristo. 22 Enyi wake, watiini waume zenu kama kumtii Bwana wetu.

Ushauri wa Paulo kuhusu unyenyekevu wa wanawake hauonekani peke yake lakini ni kwamba kila mtu katika mwili wa Kristo, wanaume pamoja na wanawake, akina baba pamoja na watoto, akina bwana pamoja na watumwa wanatakiwa "wanyenyekeane", katika kicho cha Kristo. Kwa nini katika kicho cha Kristo ? kwa sababu hivi ndivyo Yesu alivyofanya akigeuza katika utawala wa ulimwengu ambao alikuwa amepewa ili aweze kututumikia katika upendo [ angalia somo la 5] katika kunyenyekeana, tunafanya kama Yesu alivyofanya kwa hivyo tunamheshimu.

3. Je! Kuelewa huku kwa kunyenyekea kwaweza kubadilisha njia tunayo soma kifungu hiki?

Neno la Kiyunani ambalo Paulo alitumia ni ***hypotasso. Tasso*** inamaanisha kuweka. ***Hypo*** inamaanisha chini. Kutokuelewa kwingi katika yale Paulo alimaanisha alipotumia neno "kuweka chini" ni kwamba kulikuwa na hali tatu ya kuelewa kitendo hiki. Unenaji huu una wazo hili, wazo hili huitwa "sauti". Kwamba neno moja linalofana likinenwa kwa sauti hugeuza maana alizo maanisha kwa kila barua mwisho wa kila neno.

Katika Kiingereza tuna sauti mbili pekee yake. Moja ni sauti ya uwezo wetu. Katika sauti hii, "kuweka chini ya" au kukitiisha kitu inamaanisha kukiweka chini ya uwezo wetu wenyewe, kama shujaa anaweza kumutiisha adui wake chini ya mapenzi yake ***Hypotasso*** katika Waefeso 5 si sauti kama hiyo ya uwezo wa kutiisha. Kwa hakika Paulo alipowambia wakristo kunyenyekeana, mmoja kwa mwingine, hakumaanishi kwamba mwingine kwa mapenzi yake.

Katika Kiingereza sautinyingine ni sauti ya lazima. Hivi ndivyo tunaposoma mara nyingi hivi vifungu vya bibilia. Aina hii ya unyenyekevu ni kukubali kulazimishwa na mtu mwingine awe na uwezo juu yetu. Kunyenyekeana au kujitiisha katika hali ya kukubali wenyewe ni kukubali uwe adui aliyetekwa mateka, amekanyagwa chini ya miguu ya mshindi.

Lakini neno ambalo Paulo anatumia si sauti ya kulazimishwa. Lakini anatumia sauti ya kati – sauti ambayo hakuna katika Kiingereza. Sauti ya kati kwa Kiyunani ni ngumu kutafsiri katika Kiingereza. "Kila sauti ya kati ya Kiyunani ni kitendo cha kujitolea kwa mtu anayekitenda" [Bristow 1988]. ***Hypotasso*** katika sauti ya kati inamaanisha kujiweka sisi wenyewe chini ya au kujinyenyekeza mmoja kwa mwingine.

Alipotuuliza sisi kunyenyekeana, Paulo anatusihi tuache kupigania nguvu na kuongoza. Hivi ndivyo vilikuwa vita vya ulimwengu ambavyo vilikuwa vikiendelea, hata kwa bahati mbaya, katika familia- lakini haikuruhusiwa katika familia za wakristo. Kama viungo vya mwili wa Kristo, hatutakiwi kuwa juu ya watu wengine. Badala yake Paulo na Yesu walitufundisha "kuwahesabu wengine kuwa bora zaidi kuliko sisi" [Wafilipi 2:3] hata pia Petro aliandika hivi "ninyi nyote jifunzeni unyenyekevu, mpate kuhudumiana-----] [Waraka wa kwanza wa Petero 5:5.] Na tunafanya hivi "katika kicho cha Kristo"[Waefeso 5:21]- kwa sababu hii ndiyo nidhamu ya kweli ambayo Yesu alionyesha katika njia zake zote. Ijapokuwa alikuwa Bwana wetu, alituosha miguu yetu michafu.



© Carrie A. Miles, 2012

Wakati wote Paulo anaandika“jinyenyekesheni” kwa mtu mwingine, anatukumbusha kuhusu mafundisho ya Yesu, kuwa wakristo hawatakiwi wajishugulishe katika kupigania kuwa juu ya watu wengine kama ilivyo katika ulimwengu.

Kuchanganyikiwa zaidi huletwa na neno hili “kama kumtii Bwana wetu.” Wakati mwingi tunaposoma hii ni kama Wanawake wanahitaji kuwatii Waume zao kama Wanaume wao Mungu. Wakolosai 3:18 inaondoa kuchanganyikiwa huku. “Ninyi wake, watiini waume zenu, kama ipendezavyo katika Bwana.” Wanawake huwatii Wanaume wao kama sehemu ya wakristo kumwiga Yesu.

Nyakati zote wanaume wamefundishwa kuwa wana kazi ya kuwatiisha Wanawake waasi na watoto. Wanafilosofia wanawasihi Wanaume Wayahudi na Warumi “wawatawale” wake zao. Hali ya kawaida huwalazimisha Wanaume kuwa watawala pia huchangia tabia hii. Lakini katika Agano Jipya, mtu mmoja pekee yake anaye “vitia vitu vyote chini” yake ni Mungu. [Waefeso 1:22, Kamusi ya Thiologia ya Agano Jipya]

4. Je! Huku kuelewa kuwa wanawake wanastahili kujinyenyekeza kwa waume zao kunalingana na kuumbwa kwa Mwanamke kama “msaidizi wa kufanana”? au msaidizi anaye mfaa Mwanamume (angalia Somo la Kwanza)

## Umejifunza nini / changa moto za kitamaduni

5. Je! Kunayo njia nyingine ambayo uhusiano wako unaweza kubadilishwa kama ninyi wote mume na mkeo mnanyenyekeana mmoja kwa mwingine katika kumuiga Kristo (waache kujaribu kufuata njia yao yenyewe)

6. Katika 1 Wakorintho 11:7, Paulo anandika kwamba mke ni utukufu wa mumewe. Katika Waefeso 5:26-27, anawambia Wanaume wawafanye wake zao watukuzwe. Je! Wachumba watakuwa na tabia gani ili mwanamume amsaidie mkewe atukuzwe asiwe na hofu kwamba mkewe atakuwa juu yake?



© Carrie A. Miles, 2012

# SOMO LA 13 SIRI YA NDOA

Huu msururu wa masomo ulianzishwa na tamko la Yesu kwamba uhusiano wenyewe kati ya Mume na Mke ulitakiwa upatikane “katika mwanzo”, wakati Mungu alipotuumba tuwe “mmoja”. Somo letu la kuumbwa lilituletea wazo kuwa wanadamu wa kwanza walikuwa uchi na hawakuona haya” wakifurahia uhusiano wa kweli, usio na hofu, uliokubalika na kujitolea.

Mtume Paulo anasema kuwa ndoa ni mfano wa uhusiano ulio kati ya Kristo na Kanisa. Anasema kuwa ni “siri kubwa”. Je! Watu wawili wanaweza kuwaacha jamii ya wakristo na kuwa mmoja? Kama Mwanzo 2 ni mfano wa uhusiano wenyewe kabla ya dhambi, katika waefeso 5 Paulo anatuonyesha kurejea katika umoja katika ukombozi wa kikiristo.

## Unyenyekevu wa ukomavu

### WAEFESO 5 :20 - 33

20 na kumshukuru Mungu baba siku zote kwa mambo yote, katika jina lake Bwana wetu, Yesu Kristo, 21 hali mnanyenyekeana katika kicho cha Kristo. 22 Enyi wake, watiini waume zenu kama kumtii Bwana wetu, 23 kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha Kanisa, naye ni mwokozi wa mwili.24 lakini kama vile Kanisa limtiivyo Kristo vivyo hivyo wake nao wawatii waume zao katika kila jambo

25 enyi waume wapendeni (***Agape*** katika Kiyunani, inamaanisha kuwa na hali ya kutunza) wake zenu, kama Kristo naye anavyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake. 26 ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji na katika neno, 27 apate kujiletea Kanisa utukufu lisilo na ila wala kunyazi wala lolote kama hayo, bali liwe takatifu lisilo na mawaa. 28 vivyo hivyo imewapasa wanaume nao kuwapenda wake zao kama miili yao wenyewe. Ampendaye mkewe hujipenda mwenyewe, 29 maana hakuna mtu anayeuchukia mwili wake po pote bali huulisha na kuutunza, kama Kristo naye anavyolitendea Kanisa.30 kwa kuwa tu viungo vya mwili wake, 31 kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake na mama yake, ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili mmoja. 32 siri hiyo ni kubwa, ila mimi nanena habari ya Kristo na Kanisa, 33 lakini kila mtu ampende mkewe kama nafsi yake mwenyewe, wala mke asikose kumstahi mumewe.



© Carrie A. Miles, 2012

1. Ni nani anayeongelewa katika kifungu hiki cha 20-21?

2. Katika vifungu vya 25-30 Paulo anaeleza jinsi tabia ya wanaume inavyotakiwa iwe kumwelekea mkewe. Katika maisha yetu ya kila siku. Mwanamume atafanya nini katika tendo au tabia ya mambo haya kwa mkewe?

- "Ajitoe" kwa ajili ya mkewe
- Amtakase kutoka kwa mawaa yote.
- Ampende mkewe kama anavyojipenda yeye mwenyewe / mwili wake
- Amlishe na kumutunza mkewe
- Awaache baba yake na mama yake naye aunganishwe na mkewe.

Katika vifungu 22-24 na 33 Paulo anaeleza tabia ya mwanamke mkristo kumuelekea mumewe. Bristow anaandika "Paulo-------aliwauliza wanawake kwa kujitolea, kupenda kwa nia, wakubali wawe chini ya waume zao-------hii ni kwa mtu anayejitolea mwenyewe katika hali yake, "ujinyenyekeze kwa" ni tafsiri mbaya wakati mwingi (neno) humaanisha kama "kujitolea kwa" "kujiweka kwa mahitaji ya" "uwe msaidizi wa" au "uwajibike kw"'

3. Katika maisha yetu ya kila siku, ni jinsi gani au ni kwa njia gani mke:

- Aweza kutoa heshima (msaada) kwa mumewe?
- Aweza kuonyesha usaidizi wake katika kila hali?
- Amheshimu mumewe?

4. Itakuwa ni vigumu kwa mwanamume kufanya kama vile Paulo anavyosema kama mwanamke atamchezea mumewe au kumchukuwa hivi hivi. Je! Mke atawezaje kufanya mumewe amtunze kama Kristo alivyolitunza Kanisa?

## MATHAYO 19:4-6 NA MWANZO 2:24-25

(Yesu ) akajibu, akawambia, hamkusoma ya kwamba yeye aliyewaumba mwanzo, aliwaumba mtu mume na mtu mke akisema, ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili mmoja. Hata amekuwa si wawili tena bali ni mwili mmoja. Basi aliowaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe. (Mathayo)

24 Kwa hivyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe nao watakuwa mwili mmoja, 25 nao walikuwa uchi wote wawili, adamu na mkewe, wala hawakuona haya (Mwanzo)



© Carrie A. Miles, 2012

5.  Uhusiano wenyewe kati ya mume na mke kulingana na Yesu ni upi? Ni nani ambaye Yesu anasema alitangulia kusema haya?

Paulo anasema wazo hili tena katika waefeso 5:31

6.  Mwanzo 2:24-25, pia inatuambia kuwa mwanamume na mwanamke walikuwa "uchi na hawakuona haya" inamaanisha nini kuwa na uhusiano ambao mtu anaweza "kuwa uchi na haoni haya"?

7.  Linganisha uhusiano ambao mtu anaweza "kuwa uchi na haoni haya" na kueleza kwa Paulo kuhusu mwanamke na mwanamume katika Waefeso 5.

Wasomi wengi wanasema kwamba Paulo alikuwa mtetezi mkubwa wa "utawala" (jinsi vitu vilivyokuwa) na maandishi yake ya Waefeso 5-6 yalikuwa yanawahakikishia watawala wa Kirumi ya kwamba wakristo walikuwa wananchi wazuri waliotetea uongozi wa utawala ambao Warumi waliuthamini sana. Hawa wasomi wanaona kukubaliana kwa maandiko ya Paulo na wajiitao Sheria za nyumba iliyoandikwa na Wayahudi na wanafilosofia wa Kirumi, waliowashauri wanaume katika kazi yao ya kuwatawala wake zao, watoto, na watumwa ambayo iliwahitaji wanaotawaliwa kuwatii wanaowatawala. Kama Paulo alikubaliana na hawa wandishi wa Sheria za nyumba katika Waefeso 5 na 6 alitumia hayo maandiko kubadilisha sheria za nyumba juu chini. Katika nyumba ya Paulo, wanaume hawaambiwi kuwatawala wake zao, lakini wajitoe wao kwa wake zao, lakini wakubaliane nao katika amani na umoja.

Waefeso 5:21-33 haizungumzi kuhusu cheo na mamlaka. Lakini ni mausia jinsi ya kudai lengo la wanadamu "mwili mmoja uchi na hawaoni haya" huu ndio uhusiano wenyewe katika mwanzo, uliorejeshwa na Yesu na kuhubiriwa  na Paulo. Kurejeshwa kwa Mungu katika Kristo, si mmoja tu lakini tunageuzwa tuwe bila hofu, ukweli na kutoa tukiweza kunyenyekeana mmoja na mwingine katika kicho cha Kristo. "Hapo ndipo tutaweza kuhisi "siri" ya wawili kuwa mmoja.

## Umejifunza nini

8.  Kumbuka kuwa ndoa wakati wa Paulo ilikuwa ndoa ya kutengenezwa na mtu mwingine, kama ilivyo katika Africa (na katika sehemu nyingine). Je unawezaje kuwa mmoja na mtu ambaye wewe haukumchagua?

9.  Utakuwa karibu vipi katika "umoja" katika uhusiano wako na wakristo wengine? Je unaamini hii inawezekana? Ni nini husimama kati yako na uhusiano wenyewe?



© Carrie A. Miles, 2012

# WALIOCHANGIA


S. Scott Bartchy, MALLON CHRESAI: First Century Slavery and the Interpretation of 1 Cor. 7:21. Atlanta, Georgia: Scholars Press, 1973.

S. Scott Bartchy, "Issues of Power and a Theology of the Family," Mission Journal, July-August, 1987, Vol. 21, No. 1.

S. Scott Bartchy, audiotape, "Jesus, Power, and Gender Roles," and accompanying handout. Sunstone Symposium, Salt Lake City, Utah, 1993.

S. Scott Bartchy, "Undermining Ancient Patriarchy: The Apostle Paul's Vision of a Society of Siblings," *Biblical Theology Bulletin*. Vol. 29, no. 2, 1999, pp 68-78.

Gary S. Becker, *A Treatise on the Family.* Cambridge, MA: Harvard University Press, 1981.

Black, Susan Easton, "Discerning the Details, BYU Magazine Spring 2011, p.

Gilbert Bilezikian, *Beyond Sex Roles*. Baker Book House, Grand Rapids, MI, 1985.

Katherine Bushnell, *God's Word to Women*, Oakland, CA: published by the author, 1923.

Richard Cervin, "'Does *kephale* (head) mean 'source' or 'authority over' in Greek literature? A rebuttal." *Trinity Journal* 10 NS 1, 1989.

Joy Elasky Fleming, *Man and Woman in Biblical Unity*. Minneapolis, MN: Christians for Biblical Equality.

David Freedman, "Woman, a Power Equal to Man," *Biblical Archaeology Review 9*, no. 1 [January-February 1983]:58.

Ellen Gruenbaum, *The Female Circumcision Controversy: An Anthropological Perspective.* Philadelphia: University of Pennsylvania Press, 2001.

Jane I. Guyer, "Female farming in anthropology and African History," in *Readings in gender in Africa*, Andrea Cornwall (ed.), Indianapolis, Indiana: University of Indiana Press, 2005, 103-110.

Laurence R. Iannaccone, *Women and the Word of God.* Unpublished manuscript, 1980.

Craig S. Keener, *Paul, Women and Wives*. Peabody, MA: Hendrickson Publishers, 1992.

Gerhard Kittel, editor. *Theological Dictionary of the New Testament*. Translated by Geoffrey W. Bromiley. Wm. B. Eerdmans Publishing Company, Grand Rapids, Michigan, 1964.

Lesly F. Massey, *Women and the New Testament: An analysis of scripture in light of New Testament Era Culture.* Efferson, NC: McFarland and Company, 1989.

Wesley J. Perschbacher, editor. The New Analytical Greek Lexicon. Peabody, MA: Hendrickson Publishers, 1996.

Heinrich Schlier, "*Anakephalaiosomai.*" in Gerhard Kittle, editor, *Theological Dictionary of the New Testament*. Grand Rapids, MI: Wm. B. Eerdmans Publishing Company, 1965, p. 681-2.

Rodney Stark, *The Rise of Christianity*, Princeton University Press, 1996.

James Strong, *Strong's Exhaustive Concordance*. Tulsa, OK: American Christian College Press, no date.




© Carrie A. Miles, 2012